# *MTU ALIYE KATILI KULIKO WOTE SANTA MARIA*

Asante, Ndugu. Na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu sasa kwa ajili ya maombi. Nami ninaona wengi wenu mnaleta leso za kuombewa. Sasa, tu—tunaamini hilo. Baadhi ya mambo makuu sana tuliyo nayo ya kutukia katika siku hizi ni huduma ya kimataifa ya kuombea leso. Mambo makuu yanatukia, nasi tuna furaha sana kwa ajili yake. Daima tunafurahia kufanya lolote tuwezalo kuwasaidia wengine. Nami ninataka kila mtu ainame pamoja nami sasa, kisha tutaomba.

2 Baba yetu wa Mbinguni, tuna furaha, usiku wa leo, kuwa hai, na kuwa hapa katika ibada ya Mungu wetu tukiwa na hakikisho hili lililobarikiwa la kujua, kwamba wakati maisha haya yatakapokwisha hapa, tunaingia katika ule Uzima mkuu huko mbali, ambapo matarajio yetu yote yanatulia. Na wakati tukiwa katika safari hii, Bwana, maradhi, shida, huzuni zimetanda kote njiani. Na kuna wengi wanaoteseka na mambo haya katika siku hii tunayoishi, katika vivuli vya Kuja kwa Bwana. Tunajua ya kwamba adui anaenda huku na huku kama simba angurumaye, akimeza kile awezacho, kwa kuwa anajua muda wake ni mfupi.

3 Na sasa, watu wengi wameleta leso zao na kuziweka hapa kwa ajili ya wapendwa wao. Hapana shaka, huko nje kupitia jangwani kule, mahali fulani kuna maskini baba na mama kipofu, wakingojea usiku wa leo, leso ipate kurudi; labda hospitalini kuna mpendwa mgonjwa sana, mtoto mchanga wa thamani nyumbani; na Wewe unamjua kila mmoja wao, Bwana. Nami nina hakika ya kwamba Wewe utawajalia haja yao, ninapoziwekea tu mikono yangu, Bwana, katika njia ya uwakilishi wa Jina la Yesu Kristo.

4 Nasi tunaamini ya kwamba iliandikwa katika Maandiko kwamba walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo leso au nguo, na ilikuwa ni ishara za imani yao katika mtume huyo, amekuja miaka mingi iliyopita wala hapatikani na mauti, usiku wa leo, bali Roho wa Mungu hudumu yeye yule kwa wale wanaoamini vivyo hivyo. Nami naomba ya kwamba utatujalia kila haja.

5 Tupe ibada kuu usiku wa leo, Bwana. Uwepo Wako na uendelee kuwa pamoja nasi. Tupe shauku za mioyo yetu, nasi tunatumaini yote yatakuwa katika mapenzi Yako ya Kiungu kufanya jambo hili. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

6 Mnaweza kuketi. Wa—wakati mzuri sana wa ushirika, asubuhi ya leo, katika ki—kiamshakinywa, kiamshakinywa cha

wahudumu. Nilifahamiana na wengi wa hao ndugu ambao sikuwajua hapo kabla, ndipo nikaja kugundua, mwenyekiti wetu hapa alikuwa Muarkie.

7 Nao waliniambia kama ukiwaondoa Waarkie na Waokie wote California, huna chochote kilichosalia ila jangwa, kwa hiyo, kwa hiyo kwa namna fulani ninaamini jambo hilo. Ni wangapi hapa wanatoka Arkansas ama Oklahoma, mojawapo? Onyesha. . . Hakika na—nafikiri hiyo ni kweli. Vema, nafikiri baadhi ya mioyo miaminifu sana iliyowahi kudunda iko chini ya maskini mashati hayo ya Arkansas, na Waokie.

8 Kwa namna fulani nina uhusiano kidogo na Oklahoma. Mama yangu alikuwa akiishi Oklahoma, Tulsa, alipokuwa msichana. Na—nayo Arkansas ilikuwa ni wakati mimi, kwanza, nilipoanzisha mikutano iliyokuwa huko chini Jonesboro, na Moark, na Texarkana, na kushuka hadi kwenye Ukumbi wa Ukumbusho wa Robinson huko—huko Little Rock, hadi Hot Springs, na, loo, nyingi za sehemu hizo kupitia kule, Jiji la Oklahoma, Tulsa, na baadhi ya watu walio wazuri sana.

9 Nami nakumbuka tulipoenda Jonesboro, ulikuwa mmoja wa mikutano yangu ya kwanza mikuu baada ya kuondoka St. Louis, ndipo yule msichana mdogo wa Daugherty akaponywa, jambo ambalo lilichochea St. Louis nzima. Huko tulikuwa na makumi ya maelfu ya watu waliokusanyika.

10 Tukaenda Arkansas, na ilikuwa mara ya kwanza kwenye matangazo, ambapo niliwahi kuwa kwenye matangazo. Nalo gazeti likasema, ninaamini, kulikuwa na watu elfu ishirini na nane waliohudhuria huo mkutano. Walitoka kote nchini, kwa maili arobaini mzunguko ilikuwa vigumu kupata mahali pasipokuwa pamepigwa mahema na kila kitu, watu pamoja na watoto wao wamelala chini ya malori ya pamba yaliyochakaa na kujifunika vipande vya nguo huku mvua ikinyesha.

11 Kamwe sitasahau usiku mmoja kule. Ninajua sitaki kuanza kutoa shuhuda usiku wa leo. Ningeninii. . . Nikitoka. . . Niliwaambia nitawaombea wote kabla hawajaondoka, lakini hakika ilinibidi kulighairi, wao. . . wengi sana, hata usingeweza kufika karibu na. . . nayo iliendelea tu kuongezeka zaidi na zaidi. Mstari ungefikia majengo kadhaa ya mji.

12 Nami nakumbuka usiku mmoja nilikuwa nimetoka kwenda kumwombea mtu fulani. Walikuwa wameshuka kutoka. . . Asubuhi hiyo nilikuwa nimeomba usiku kucha nikisimama, nikapiga magoti, nisingeweza kusimama tena, huku nimepiga magoti tu, nikiwaombea wanapopitia.

13 Basi kulikuwako na fundi viatu, kipofu, kutoka mahali fulani huko juu, nasahau jina la mji huo sasa, karibu na Jonesboro, yapata maili thelathini, arobaini, alikuwa kipofu kwa miaka kadhaa, naye Roho Mtakatifu alikuwa amemtangaza

amepona. Ndipo akazunguka, akarudi mstarini tena, kasema, “Ulisema, Bwana, niliponywa, macho yangu hayajafunguka.”

Nikasema, “Hilo halina uhusiano wowote nalo, uliniambia uliniamini.”

Akasema, “Nakuamini.”

Nikasema, “Basi kwa nini unaniuliza swali?”

Na kwa hiyo, akasema . . . akaendelea; nami nikasema endelea tu kusema, “Bwana asifiwe kwa ajili ya macho yangu.”

14 Naye alikuwa akienda nyumbani asubuhi hiyo, yapata saa kumi na moja, akiendeshwa na, ninaamini ilikuwa ni mwanawe, kwenye ga—gari kuukuu la Muundo A, wakipanda barabarani. Naye alikuwa ameketi kwenye kiti cha nyuma akisema, “Bwana asifiwe kwa ajili ya macho yangu,” ndipo macho yake yakafunguka. Naye karibu aishtushe nchi nzima.

15 Na kwa hiyo, akaingia mbio kwenye kanisa Katoliki asubuhi hiyo huku kofia yake ikiwa nchani mwa fimbo yake, akiizungusha tu namna *hii*, akimsifu Mungu kwa kufunguliwa macho yake. Kisha akaenda huko katika kanisa la Methodisti, nao walikuwa wakitaka akamatwe kwa sababu ya kuvuruga ibada. Haionekani kana kwamba hiyo ingeweza, ilivuruga chochote, bali—bali ingeninii . . .

16 Basi usiku huo, nilikuwa tu nimezunguka nikaingia jukwaani, ndipo nikaona mabawabu fulani wakiniashiria, na palikuwa na dereva pale, akasema, “Nina safari mbili zaidi za kufanya usiku wa leo, kuwaleta watu kutoka hospitalini.”

17 Nikatoka nje kuninii . . . nikapita ili kuwaombea baadhi . . . mwanamke aliyekuwa huko nje ambaye alikuwa, walidhani alikuwa akifa kwa kansa. Naye alikuwa ameuza matunda meusi aliyokuwa ameyatia koponi apate gari la kuchukulia wagonjwa kumleta huko, mumewe alifanya hivyo. Hizo ndizo karibu zote walizokuwa wamesalia nazo, wakatengeneza mifarishi kadhaa, nao walikuwa . . . akauza hiyo. Bwana akamponya, akasimama akatoka kwenye hilo gari la kuchukulia wagonjwa, akatokea nyuma, akaingia ndani, akajaribu kufika kwenye mkutano.

18 Nami nisingeweza kurudi mlangoni tena, kulikuwa na wengi sana waliolundikana mle ndani hata, yapata umbali wa *hili*, kuta hadi ukuta, nami nisingeweza kujipenyeza na kupita. Ndipo mmoja wa mabawabu akaja, akasema, “Tutakuchukulia nyuma ya hili jengo, hakuna mtu anayekujua.”

19 Nilikuwa huko yapata siku nane ama kumi, wala hakuna mtu bado aliyekuwa—aliyekuwa ameninii . . . Wengi walikuwa wameingia mahali hapo. Wangekaa huko mchana na usiku, wakingojea tu zamu yao. Kwa hiyo basi nikazunguka upande wa nyuma, nami ninakumbuka ikianza, kidogo ikaanza kunyesha, nami karibu nisingeweza kujipenyeza katikati ya huo umati,

huku nikijaribu kufika kwenye mlango wa nyuma ambapo wananichukua nipate kufika jukwaani tena.

20 Ndugu zangu weusi, dada usiku wa leo, samahani kwa tamshi hili, na jinsi nitakavyolisema. Lakini ilikuwa, katika siku hizo, wangali walikuwa na namna fulani ya ubaguzi huko Arkansas. Kwa hiyo nikaanza kuingia, ndipo nikasikia... mtu fulani akimwita baba yao, nami nikaangalia, alikuwa ni msichana mweusi mwenye sura nzuri, alikuwa kipofu. Alikuwa akijipenyeza huku na huku kwenye umati, akimlilia baba yake. Nami...Hakuna mtu aliyekuwa akimjali msichana huyo.

21 Wala hakuna mtu aliyenijua, kwa hiyo nikaanza kusukuma namna *hii*, nami...jamaa fulani wamesimama tu pale wakizungumza. Kulikuwa na mabasi kadhaa ya kukodiwa pale kutoka sehemu mbalimbali za nchi. Kulikuwa na jamaa aliyesimama pale, akipiga kelele, akiongea, nami nikajaribu kujipenyeza karibu naye.

Akasema, "Acha kusukuma."

Nami nikasema, "Naam, Bwana." Na kwa hiyo nikaanza kusukuma tena.

Naye akasema, "Nilisema, 'Acha kusukuma!'"

Nilihofia ataanza kusukuma, kwa hiyo nikasema, "Samahani, Bwana." Kwa hiyo nikazunguka upande huo mwingine.

Basi hatimaye, nikaingia kwenye mkondo wa msichana huyo. Ilisikika kama mnafiki kufanya hivyo, lakini nilifika pale pale mahali alipokuwa akisukumia.

Naye angesema, "Mtu anisaidie. Mtu anisaidie."

Nami nikaendelea tu kusonga mbele, mwajua, mpaka akanigonga.

Akasema, "Samahani, *Pwana*."

Nami nikasema, "Unataka nini?"

Akasema, "Waweza kunisaidia kumtafuta baba yangu?"

Nami nikasema, "Unataka nini na baba yako?"

22 Akasema, "Vema, nimekuja hapa kumwona huyo *mponyachi*." Kisha kasema, "Wananiambia ya kwamba hata siwezi kulikaribia hilo jengo. Nami nimempoteza baba ya—yangu, wala siwezi kupata njia ya kurudi kwenye basi."

Nikasema, "Unatoka wapi?"

Naye akasema, "Memphis."

Basi nikaangalia, ndipo nikaona basi la kukodi, nilifikiri ninaweza kumrudisha msichana huyo kule, labda. Kwa hiyo nikasema, "Ati umekuja kumwona *nani*?"

Akasema, "*Mponyachi*."

23 Nami nikasema. . .Nikawazia ningemhoji tu, nione kweli alikuwa na imani kiasi gani. Sasa, hilo linasikika kama mnafiki kwa maskini msichana kipofu. Lakini nikasema, "Ati mponyaji?"

"Naam, Bwana."

24 Nami nikasema, "Usiseme kwamba unaamini kitu kama hicho, siku kama hizi, jinsi tunavyoishi kimamboleo siku hizi, tukiwa na madaktari wengi na kadhalika? Huku nawe unaniambia ungeenda kusikiliza kitu kama hicho?"

Akasema, "Bwana, hawawezi kunisaidia."

Nami nikasema, "Kumbe." Nikasema, "Ni nini kilichokupa wazo la kuja hapa?"

25 Anasema, "Mimi husikiliza redio, na vipindi vyote vizuri." Kisha akasema, "Nilikuwa nikisikia kutoka hapa Fayetteville," huko ndiko alikotoka mtu huyo, Fayetteville. Akasema, "Nilisikia matangazo kutoka Fayetteville," nayo yakasema, "mtu aliyekuwa kipofu, mshona viatu, alifunguliwa macho hapa asubuhi ya leo." Kisha kasema, "Sote tulikusanyika tukaja hapa kwa basi la kukodi." Kisha kasema, "Waweza kunisaidia kurudi?"

Nikasema, "Naam, Mama. Lakini," nikasema, "kwanza, unaonaje kuhusu hilo?" Nikasema, "Huamini mtu huyo angeweza kufanya hivyo?"

Akasema, "La, bwana." Akasema, "Lakini Yesu anaweza kufanya hivyo."

Nami nikasema, "Hmm!" Nami ni—nikasema, "Vema, sikiliza, kweli unaamini hilo?"

26 Akasema, "Bwana, hebu nikwambie utakalofanya." Akasema, "Kama utanisaidia kuingia mahali alipo, basi ninaweza kumpata baba yangu baada ya hapo." Loo, nena kuhusu kemeo! Akasema, "Nisaidie kufikia mahali alipo, nitampata baba yangu baada ya hapo."

Nikasema, "Mama, unamaanisha hilo?"

Akasema, "Naam, Bwana, ninamaanisha."

Nami nikasema, "Labda mimi ndiye unayetaka kumwona."

Ndipo akanishika namna *hiyo*, nayo mikono yake ikalishika koti langu, ndipo akasema, "Wewe ndiye yule *mponyachi*?"

Nami nikasema, "La." Nikasema, "Mimi ni Ndugu Branham."

Akasema, "Huyo ndiye ninayetaka kumwona." Naye akasema, "Kama utamwomba Mungu, nitampata baba yangu."

27 Nikamtazama amesimama pale, macho yake meupe, yakipepesuka, machozi yakitiririka mashavuni mwake, nami nikawazia juu ya kipofu Fanny Crosby:

Usinipite, Ee Mwokozi mpole,
Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

28 Mnaona? Alikuwa amesikia habari za yule kipofu kufunguliwa macho. Naye akasema daktari alimwambia ya kwamba watoto wa macho walipaswa kuiva, ndipo wangeweza kufanya upasuaji. Lakini sasa, baada ya kuiva, walikuwa wamejizungusha kwenye neva ya macho ama chochote kile, wala hapakuwa na matumaini kwake. Naye akasema, "Matumaini yangu pekee ni kuingia."

29 Nami nikamshika tu mkono, nikasema, "Baba wa Mbinguni, miaka mingi iliyopita kulikuwako na msalaba wa kale ulioparuza ukikokotwa kupitia Yerusalemu, mitaani, ukikokota nyayo zilizojaa Damu ya huyo Mbebaji. Akienda Zake kilimani, maskini mwili Wake dhaifu, mnyonge, ukaanguka chini ya huo mzigo, kulikuwako na Simoni, Mkirene, aliyekuja na kuuchukua huo msalaba akamsaidia kuubeba." Nikasema, "Huyu hapa mmoja wa watoto wake usiku wa leo, akiyumbayumba gizani, Bwana, nina hakika Wewe unaelewa." Akaanza kumsifu Mungu, angeweza kuona. Hakukuwa na lingine. Aliweza kuona.

30 Kumekuwa na mambo makuu yaliyotukia huko Arkansas, tunashukuru sana. Nyingi za shuhuda hizo, nyakati za kale, nadhani nitakapovuka kile kizimba, mimi. . .kutakuwa na nyingi nitakazosikia. Mimi. . .Mambo mengi sana yanakuja niani mwangu kuhusu siku hizo za kale, na kote katika miaka, na kote kwenye bahari ya shuhuda popote unaposimama.

31 Mtu fulani, asubuhi ya leo mkutanoni, mchungaji hapa, mkewe, ameketi *hapa*, alikuwa akiniambia yapata mara tatu ambapo Bwana amemwita mikutanoni namna hiyo. Naye aliponywa ugonjwa wa Hodgkin, huo ni kansa, mwajua, iko kwenye tezi. Kwa hiyo wao. . .Na mambo mengi yalikuwa yamefanywa.

32 Ndugu mwingine, akisimama pale akishuhudia, hivi majuzi tu, huko juu katika mji mwingine, juu ya kansa iliyojaa usoni mwake, naye Mungu alikuwa amemponya. Hata nisingeweza kuona alama yake popote; na mambo mbalimbali, na kila mahali uendapo inaonekana hivyo.

33 Sasa, usiku wa leo utakuwa ndio usiku wa mwisho ambao watakuwa wakiuza vitabu hivyo na hizo picha ndogo. Sisi si wauza vitabu, hatuko hapa kuuza vitabu. Vitabu hivi vinanunuliwa kutoka kwa mtu mwingine, kisha vinaletwa mkutanoni, rafiki yangu mwema anaviuzia mlangoni. Hatuuzi Jumapili, tunaiacha siku hiyo wazi. Kwa hiyo sisi. . .Kama ungevitaka, ama mojawapo ya hizo picha, mbona, unaweza kuzipata mlangoni unapotoka, kama hujavipata bado (Kesho ni Sabato.), na pia, katika kanda, nina hakika zimetangazwa hapa.

34 Sasa, katika mkutano huu, sijajaribu mahubiri yoyote, kwa sababu nilijua ya kwamba hii ilikuwa ndiyo mara yangu ya kwanza hapa; nimejaribu kulifanya rahisi tu liwezavyo kuwa. Lakini Bwana ametupa jumbe kuu, mamia na mamia ya hizo zilizo kwenye kanda, kama vile *Nyakati Saba za Kanisa*, *Mwa—Mwa—Mwanzo Wa Ule Uzao,* na *Ninii*, loo, *Mwana-Kondoo na Hua*, na *Kushuka Kutoka Utukufuni Mwake*, na—na kila namna ya—ya jumbe ambazo—ambazo—ambazo ni... Nafikiri Bwana alibariki. Nao wanazo hapa, nanyi mlio na vinasasauti mngeweza tu kumwona Bw. Maguire hapa, na mfurahie kuzipata.

35 Nami nilikuwa nikimwambia mchungaji leo, hatutaki kamwe kuweka mkazo wowote wa pesa. Nina umri wa miaka hamsini na mitatu, nimekuwa nikihubiri miaka thelathini na miwili, wala sijachukua sadaka yangu ya kwanza bado. Sijawahi kupokea sadaka maishani mwangu, wala si—sifanyi hivyo. Ninaninii tu...Matumizi yanapolipiwa, hilo latosha.

36 Nimeona wakati ambapo tungechukua siku mbili usiku, tukichukua sadaka, na wakati ambapo ungeweza kupitisha mfuko wa sadaka na kupata dola elfu saba, halafu mara tu matumizi yanapolipiwa, nisingewaruhusu kuchukua senti nyingine, hivyo tu. Siamini kabisa kufanya hivyo. Nami nilisema wakati wowote ambapo matumizi hayajatosha, nijulishwe tu, kanisa langu nyumbani litalipia yaliyosalia.

37 Nasi tunataka mjue ya kwamba hatuko hapa kuchukua pesa. Hatuko hapa kwa ajili ya chochote ila kujaribu ku—kushiriki pamoja nanyi, na kurahisisha mizigo kidogo, na kuwaombea wagonjwa, na kufanya yote tuwezayo kuwasaidia wakati tukiwa hapa.

38 Na sasa, kesho ni Sabato, na sasa, ninyi watu mnaotembelea hapa, kuna makanisa mazuri sana hapa. Hawa hapa wachungaji wao na...wameketi hapa. Sasa, hudhurieni baadhi ya makanisa yao, wao ni watu wa Mungu, wanaamini katika huduma hii. Nayo ni madhehebu mbalimbali, lakini sisi hatufanyi hivyo, ikija ni ushirika pamoja na Kristo, hatuweki mipaka yoyote ya kimadhehebu, tunaenda tu pamoja.

39 Niliwekwa wakfu katika kanisa moja, Baptisti ya Kimishenari, kamwe sijawekwa wakfu katika kitu kingine chochote. Nami huja tu miongoni mwa watu kama ndugu, kusimama na kuunganisha, jamani, loo, njia kati ya udugu. Kama ningeweza kuona kila kanisa likisahau tu ninii yake, mpaka wake wa kimadhehebu, na kuingia tu kama udugu mmoja mkubwa, ningesema kama Simeoni wa kale, "Bwana, mruhusu mtumishi Wako aondoke kwa amani, kwa kuwa macho yangu yameuona wokovu Wako." Hiyo ni kweli. Wakati sote tungeweza kukusanyika namna hiyo, mimi...hilo ndilo sikuzote nimeshindania.

40 Sasa, hatutaki kuwaweka muda mrefu kupita kiasi. Kwa hiyo ninyi. . . Singejali mkikosa kufanya kazi ya siku moja, mwajua, katika siku ya juma, lakini hakika sitaki mwikose shule ya Jumapili asubuhi. Sasa, kamwe usifanye hivyo. Kwa hiyo nitawaruhusu muondoke mapema bila shaka usiku wa leo, kusudi mhakikishe kuwa mtahudhuria shule ya Jumapili asubuhi. Na hiyo ndiyo shule kubwa kuliko zote ulimwenguni.

41 Na sasa, ninataka kuwaambia jambo fulani kuhusu shule ya Jumapili: Ni kosa kabisa kuwatuma watoto wenu kwenye shule ya Jumapili, mnajua hilo, wapelekeni. Hiyo ni kweli. Naam, sisi. . . Mtoto. . .

42 Niliona katuni ndogo gazetini, si muda mrefu uliopita, ilikuwa ya ajabu sana. Mvulana mdogo alikuja mlangoni, alikuwa. . . ilionyesha chumba cha kulala cha mama na baba yake, chupa zimetapakaa sakafuni, na vipande vya sigara juu ya kila kitu. Na muda umeenda sana mchana, saa tatu, naye huyo mvulana mdogo alikuwa tayari ameamka, na kuoga, na—na kuchana nywele zake, akavaa nguo zake, na kubisha mlangoni, na kusema, "Aisee, ni nani atakayenipeleka kwenye shule ya Jumapili?" Haya basi. Hivyo karibu ndivyo mtindo wa Marekani ulivyo. Si ni jambo baya sana?

43 Hebu wazieni juu ya Wamarekani wa kisasa. Ni kitu gani? Vema, baba yuko chini kwenye chumba cha kamari, na mama yuko huko nje pamoja na shirika kipenzi mahali fulani, amejianika ufuoni, binti yuko chini kwenye kantini, ama huko chini kwenye roki, Kadogoo ana gari la mbio huko nje mtaani, anatimua mbio. . . Haya basi. Hiyo ni. . . Mtu ananunua hambaga, hakuna maisha ya nyumbani, hakuna maisha ya maombi.

44 Daima nimesema jambo hili, "Ukinyosha. . . Tunapovunja uti wa mgongo wa Marekani, ni wakati umama unapovunjika." Nami na—nasema hili kwa heshima ya kiungu kwa dada zangu. Asubuhi ya leo nilikutana na baadhi ya wanawake wazuri sana kule. Lakini imekuwaje kwa wanawake wetu? Mwanamke ana shida gani?

45 Niliingia kwa Clifton hapa si muda mrefu uliopita. Asubuhi moja nikimngojea Ndugu Arganbright, tulikuwa tunaenda kula kiamshakinywa chao. Ndipo msichana mmoja akaingia mle ndani, nami ni—nikamwangalia. Nami. . . Alikuwa na mojawapo ya mitindo hii hapa ya kukata nywele kichwa-maji, mwajua, kama Ma—Mama Taifa, mwajua, nami na—nafikiri hiyo ni sura ya kinyama sana. Ndipo nikamwangalia, naye alikuwa ni kijani, sehemu moja ya macho yake, na sehemu ya pili ilikuwa bluu, na kote usoni mwake kulikuwa na kitu fulani.

46 Nami ni—ni—nikamsikitikia, nilifikiri kwamba alikuwa na shida fulani. Nami nikasimama pale, na ni—nilitaka kumwendea na kumwambia ni—ni—nilikuwa mmishenari,

ni—nimeona upele, nimeona ukoma, nami. . .lakini sijawahi kuona kitu kama hicho. Nami ni—nilitaka ku—kumwuliza kama nisingeweza kumwombea, kumsaidia, ndipo akaja msichana mwingine akiwa vivyo hivyo, nami nikawazia, "Usiniambie ya kwamba wanawake wazuri wangeninii, ambao kweli ni ki—kipawa kwa wanaume, na watauwa, na—nao wangetaka kuwa. . .kujigeuza uso, na kujifanya waonekane kama kitu fulani kutoka kwenye. . .kilichoanguka kutoka kwenye mkokoteni wa mzishi, ama chochote kile." Na—na—nashangaa tu jinsi ambavyo kamwe wangepata kitu kama hicho.

47 Na wanawake wetu wa Kipentekoste namna hiyo, hiyo—hiyo ni mbaya sana; hiyo ni—hiyo ni mbaya sana, aibu, dada. Kuna kuachilia mahali fulani, natumaini sio mimbarani. Kumbuka jinsi mwanamke anavyopaswa kuwa, yeye ni mzuri sana.

48 Nilikuwa nikizungumza na mtu fulani leo. Wakati Rebeka alipokuja kukutana na Isaka, hivi mliona aliufunika uso wake? Wa—wangali wanafanya hivyo, hawajui wanalofanya, lakini bibi-arusi huufunika uso wake. Kwa nini? Mwanamume ndiye kichwa chake. Halafu basi, yeye hana. . .yeye. . .ninii yake. . . Tabia ya mwanamke ni kujisalimisha kwa mwanamume. Na hiyo ndiyo sababu Ka—Kanisa linapaswa kutiwa utaji, lina Kichwa, Hicho ni Kristo. Hivyo ndivyo. . .

49 Wanawake wanapaswa kuwa na nywele ndefu kwa sababu ya. . .ya kichwa chake, ambacho ni mumewe; mwanamume anapaswa kuwa na nywele fupi kwa sababu ya Kristo. Mwanamke huwa na nywele ndefu kwa sababu ya Malaika. Malaika ni nini? Mjumbe, mjumbe wa kweli kwa Kanisa. Hiyo ni kweli. Daima atalikemea, aseme ni kosa, mnaona, na kadhalika. Nalo Kanisa, lijitolee sana kwa Yesu hata lisidai kichwa Chake Lenyewe, uongozi Wake Lenyewe. Kristo ndiye Uongozi wa Kanisa, limetiwa utaji, sisi sio wetu wenyewe, bali sisi ni Wake, ah, tumejitolea Kwake na Kwake pekee. Ni nzuri jinsi gani!

50 Hebu na tusome Maandiko kidogo sasa. Daima ninapenda kulisoma Neno Lake, kwa sababu neno langu ni neno la mwanadamu, litashindwa, bali Hilo ni Mungu, haliwezi kushindwa, haliwezi kushindwa kamwe. Andiko hili linapatikana katika mlango wa 7 wa Luka, kuanzia kifungu cha 36:

> *Basi mtu mmoja wa Mafarisayo alimwalika ale chakula kwake. Akaingia katika nyumba yake yule Farisayo, akaketi chakulani.*
>
> *Na, tazama, mwanamke mmoja wa mji ule, aliyekuwa mwenye dhambi, alipopata habari ya kwamba Yesu alikuwa ameketi chakulani katika nyumba ya yule Farisayo, akaleta chupa ya marimari yenye marhamu,*
>
> *Akasimama nyuma karibu na miguu yake, akilia, akaanza kumdondoshea miguu machozi yake, na*

> *kuipangusa kwa nywele za kichwa chake, akiibusu-busu miguu yake na* kuipaka *yale marhamu.*
>
> Lakini *yule Farisayo aliyemwalika alipoona vile, alisema moyoni mwake, akisema, Mtu huyu, kama angekuwa nabii,* . . .

Mimi nisome hilo tena. Sasa, sikilizeni kwa makini sana.

> Naye *yule Farisayo aliyemwalika alipoona vile,* . . . *alisema moyoni mwake, akisema,* Kama *mtu huyu* . . . *Mtu huyu, kama angekuwa ni nabii, angemtambua mwanamke* aliyemgusa *ni nani, naye ni wa namna gani: ya kwamba ni mwenye dhambi.*
>
> *Yesu* alijibu *akamwambia, Simoni, nina neno nitakalo kukuambia. Naye* akasema, *Mwalimu, nena.*

51 Kama nilikuwa nikitaka kulipa hili anwani, ningeliita: *Mtu Aliye Katili Kuliko Wote Huku* . . . Sante? Santa Ana? [Ndugu mmoja anasema, "Santa Maria."—Mh.] . . . *Santa Maria.* Ni nyingi sana Sante, Santa, Santa huku na huko hapa chini, ninazichanganya kabisa. Linamaanisha nini? Mtakatifu? ["Mtakatifu Maria."] Mtakatifu Maria.

52 Vema, hapana shaka alikuwa amechoka sana, wakati alipofika tu juu ya kile kilima akitazama kuelekea Galilaya, alikuwa akikimbia mchana kutwa, naye . . . miguu yake ilikuwa inanata kwa jasho, uso wake ulikuwa na milia ambapo lilishukia usoni mwake. Nguo zake zilikuwa zimelowa maji na zinanata alipotazama huko chini, akakata pumzi, aliona umati mkubwa umesimama karibu na Mtu fulani, akawaza, "Hakika, huyu ndiye mtu yule."

53 Mnaona, alikuwa ameenda Kapernaumu, alikuwa ameulizia, mji baada ya mji, "Je, mtu *fulani-fulani* amekuwa hapa ambaye huwaponya wagonjwa na anaitwa 'Nabii wa—wa Galilaya?'"

54 Huenda mtu fulani alisema, "Naam, Yeye alikuwa hapa juzi. Ila hatujui alikoenda, kwa sababu ameondoka, na wengi wa mjini wamemfuata." Taarifa nyingi za kumtetea na za kumpinga.

55 Angeenda kwenye mji mwingine, naye angesema, "Je, mtu *fulani-fulani* amekuwa hapa ambaye huwaponya wagonjwa, na—na kutabiri, na anajua siri za moyo? Mtu *fulani-fulani* namna hii?"

56 "Naam, Yeye alikuwa hapa jana tu, bali ameondoka. Sijui aliko wala alikoenda." Na kuendelea, na kuendelea, hiyo hadithi ikazidi kuendelea. Ndipo hatimaye . . .

57 Mnaona? Alikuwa ni tarishi, alitumwa na bwana wake, Fa—Farisayo, askofu, ukasisi wa kanisa kuupeleka ujumbe. Naye angeweza, hatimaye, angeweza kuvuta pumzi ya faraja, kwa sababu alikuwa amemwona Mtu huyo kwa mbali ambaye alikuwa amfikishie ujumbe.

58 Sasa, huo ujumbe ulikuwa muhimu sana, kwa sababu kuhani alikuwa amemtuma, huyo Farisayo. Na ilikuwa muhimu sana kwamba akutane na Mtu huyu, alikuwa ametumwa kufanya jambo hili, naye hana budi kumfikia Mtu huyu. Na hilo lilikuwa ndilo jambo kuu zaidi maishani mwake, ni kuupeleka ujumbe wa kuhani huyu, umfikie Yesu wa Nazareti.

59 Basi hatimaye, akijitahidi kushuka kilimani, baada ya kukata pumzi na kujisukumiza kwenye huo umati, hapana shaka alininii. . . Huenda ilikuwa ni Nathanaeli, ama labda ilikuwa ni Filipo, maana kwa namna fulani alikuwa ndiye mlinzi wa nje. Petro, na Luka na waandishi waliokuwa wakiandika yale aliyofanya na yale aliyosema walikuwa wamesimama karibu Naye.

60 Petro alionekana kuwa ndiye yule mvuvi mkuu mwenye nguvu, ambaye kama wangevunja m—m—mstari wa wale mitume wengine, kidogo alikuwa ni mtu mwenye nguvu, angeweza kuwasukuma nyuma na kuwaweka mbali Naye.

61 Basi tarishi huyu alipofika kwenye mstari wa kwanza wa ulinzi, huenda ilikuwa ni Filipo, naye akasema, "Lazima nimwone bwana wenu, nina ujumbe kutoka kwa bwana wangu kwenda kwa bwana wenu. Naye bwana wangu ni mtu mashuhuri, yeye ni mmoja wa watu mashuhuri sana wa jamii yetu. Yeye ni Fa—Fa—Farisayo, yeye ni tajiri, naye yuna thamani ya pesa nyingi, naye amenituma kuzungumza na Bwana wenu." Ndipo Filipo, bila shaka akitaka, kama Mkristo, kufanya yote aliyoweza ku—kumsaidia, akamleta karibu.

62 Ndipo hatimaye, akajipenyeza mpaka akakutana na Simoni, akasema, "Simoni, huyu tarishi ana jukumu muhimu sana, nami sina budi kumpeleka mbele ya Bwana." Naye Filipo akajipenyeza akamfikia Petro, akaamka. Basi hatimaye yule tarishi akaletwa uso kwa uso kwa Yesu, Huyo hapo amesimama, midomo Yake imepasuka, macho Yake yamechoka, akinena, amepwelewa na Sauti kutokana na mavumbi ya miguu ya watu.

63 Ndipo yule tarishi akasema, "Bwana, nimetumwa kukwambia ya kwamba bwana wangu amekuheshimu kwa mwaliko. Atakuwa na karamu. Atafanya dhifa kubwa, yeye hufanya hivyo kila mwaka, na—naye anakutaka uhudhurie karamu hii."

64 Angewezaje kusema jambo kama hilo? Angewezaje? Akisimama Mbele za Kristo kwa mara yake ya kwanza halafu imbidi kuendeleza biashara fulani kuhusu dini yake ya kujibunia.

65 Loo, laiti ningalisimama pale! Jambo la kwanza ningalitenda, lingekuwa ni kuanguka kifudifudi mbele Zake, na kuomba msamaha wa dhambi zangu. Lakini huo karibu ndio mtindo wa siku hizi, wakati watu wanapokutana Naye uso kwa

uso, wana mambo mengine hawana budi kuyazungumzia badala ya kuhusu hali yetu ya dhambi.

66 Basi tarishi huyu, akisimama pale, alitoa ujumbe wake. Nami ninaweza kuwazia nikimwona Bwana wetu akimwangalia huyo jamaa kwa huruma na kuwazia, labda, kwamba alikuwa akipita nafasi iliyo kubwa kuliko zote iliyopata kuwa mbele ya mwanadamu yeyote, ilikuwa ni kusimama Mbele za Yesu Kristo.

67 Huyo hapo, lakini mnaona, alikuwa amekuja katika... Mungu alikuwa amekuja katika mfano wa Mwanadamu, wala hakujua, naye huyo hapo amesimama. Ndipo Yesu, pamoja na ratiba Yake yote yenye shughuli nyingi, akiwa na maelfu ya mahali pa kwenda, na yote yaliyompasa kufanya, ninaweza kumwona katika heshima, na kama muungwana, akatikisa kichwa Chake, kasema, "Mwambie bwana wako nitakuwako."

68 Tunajifunza nini hapa? Kwamba Yeye ni...daima huja mahali anapoalikwa, hiyo ni kweli, daima huja mahali anapoalikwa. "Mwambie siku *fulani-fulani* kwamba nitakuwepo siku hiyo, kwa sababu amenialika Mimi, nitakuwako."

69 Sasa, halafu baada ya hayo, yule tarishi hapana shaka aligeuza mgongo wake, kisha akaondoka, na kuvuta pumzi ya kuridhika kwamba alikuwa amefanya jambo kubwa. Alikuwa amefanya nini? Alikuwa ameacha kitu kikuu kuliko vyote ulimwenguni kimponyoke, ile nafasi ya kuanguka miguuni pa Kristo.

70 Sijui kama wengi wetu hatufanyi hivyo. Labda tumelifanya juma hili. Huenda tukafanya hivyo usiku wa leo, kuipa kisogo nafasi ya kuokolewa, na kuwa na Uzima wa Milele, na kisha kuuacha.

71 Watu wengine wakati mwingine huwa wagonjwa, halafu wanaponywa, na kisha wanaondoka wakifikiri ya kwamba wamefanikisha jambo muhimu hasa walilolijia. Jambo bora zaidi la kulijia ni kumpata Yeye kama Mwokozi wako, ni kumjua Yeye, kwamba Yeye ni Nani maishani mwako, kuwa na uhakika.

72 Watu siku hizi ni kama watu waliopita miaka mingi iliyopita, wanajaribu kulikwepa jambo hilo. Ni kama ninii—ni kama ile mikate na samaki, alikuwa Nabii mkuu maadamu aliwaponya wagonjwa na kufanya miujiza, bali alipoanza kuwaambia Kweli, walianza kumwacha, hakuwa maarufu tena wakati huo.

73 Sasa, tunaona ya kwamba tarishi huyu alimpa Bwana Yesu kisogo. Kulingana na Maandiko, hayasemi kwamba aliwahi kuomba msamaha wa dhambi zake ama chochote kile, kisha akaondoka, akarudi kwa bwana wake yule Farisayo.

74 Sasa, kuna—kuna kasoro katika hadithi hiyo hapo, kamwe haitoshelezi. Kuna kasoro fulani, hao Mafarisayo hawakuwa pamoja na ushirika na Yesu, walikuwa hawapatani. Wao...

75 Yesu hakuwa na ushirika pamoja nao, Yeye aliwaambia, kasema, "Ninyi huzunguka bahari. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .mwongofu mmoja, halafu yeye ni mtoto wa kuzimu mara mbili zaidi ya alivyokuwa hapo awali." Akasema, "Enyi viongozi vipofu wa vipofu." Akasema, "Isaya alinena vema juu yenu. Mna macho wala hamwezi kuona, na masikio wala hamwezi kusikia." Na jinsi alivyowakemea, na—na kuwawakaripia! Na—na halafu kwa, mmoja wao kumwalika chakulani? Kama tungeliweka katika msemo wa mitaani, tunajua kuna mpango uliofichika mahali fulani, jambo fulani la siri. Mnaona? Anashikilia kitu fulani, maana hawakuwa na ushirika mmoja na mwenzake.

76 Ni kama tu unavyowachukua mu—mume na mke wakongwe na mume na mke vijana. Unawaona hao mume na mke vijana waliofunga ndoa wakienda upande mmoja na kuzungumza. Kwa nini? Wana mambo shirika. Wanapenda kuzungumza juu ya mambo waliyo nayo shirika. Waangalie watoto wadogo, wavulana wadogo watacheza gololi, wasichana wadogo watachezea wanasesere. Mnaona, ni mambo shirika.

77 Hiyo ndiyo sababu tunakutana hapa jinsi tunavyokutana, kama kile kiamshakinywa kizuri sana asubuhi ya leo. Tulikuwa na kila kitu shirika, ushirika. Wacheza kamari, wauza pombe haramu, waongo, na wezi hawakuwa na nafasi katika mkutano huo, mnaona, kwa kuwa ni, ama, hapa ndani. Sisi ni. . .Tuna ushirika mmoja na mwenzake, kwa sababu tumekusanyika kwenye ki—kitu kimoja kikuu ambacho tumefanikisha, hicho ni Kristo, ushirika pamoja Naye.

78 Sasa, unapomwona msichana mdogo mwenye umri wa kama miaka sita au saba akimfuata nyanya wakati wote, aha, kuna kasoro. Kuna tofauti kubwa mno katika umri wao. Sasa, ama yeye ni kipenzi cha nyanya, ama ana kifurushi cha peremende, na msichana huyo mdogo anakitaka. Mnaona? Kuna kusudi fulani kwa msichana huyu mdogo kumfuata nyanya, kwa sababu kuna tofauti kubwa mno katika umri wao. Mnaona?

79 Na unapowaona hawa Mafarisayo wakituma, loo, mfumo huo wa kikanisa wenye kiburi, wenye msimamo mkali, ukituma mwaliko kwa Yesu, kuna kasoro, kitu kisicho cha kawaida, kuna ujanja mahali fulani. Usifikiri Yesu hakujua jambo hilo, hakuwa akiweka chochote juu Yake. La, la. Mnaona? Alijua habari zake, lakini hata hivyo, kama alialikwa, Yeye ataenda kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli.

80 Tunamwalika makanisani mwetu, tunaalika mikutano mikuu kabla ya uamsho, na kuomba, na kuita makundi makubwa ya makundi ya maombi kwa ajili ya mkutano mkuu wa jimbo lote, uamsho, na kuomba, "Loo, Bwana Yesu, njoo u—ukatukirimie kwa Uwepo Wako." Na hebu mtu fulani asimame na kusema, "Amina," nao mabawabu watamwelekeza nje ya

mlango. Hebu mtu fulani amwabudu kidogo, nao ni kundi la walokole. Hiyo ni kweli.

81 Tunamwalika, halafu hatumtaki anapofika huko. Lakini Yeye atakuja kwa vyovyote vile. Yeye huja, loo, naam, atakuwako. Anapoahidi... Ukimwomba, haidhuru hali ya mambo ikoje, Yeye huja unapomwomba, Yupo.

82 Ndipo ninaweza kumwona Farisayo huyu, jinsi walivyoandaa mlo huu mkubwa! Walikuwa matajiri, jamani, walipata sehemu ya kila kitu kilichokuja, na sadaka ya nyama, na kulipwa vizuri, na, loo, walikuwa, walikuwa na anasa. Walikuwa... Hilo ni tamshi la kale la kusini, bali ndi—ndilo walilofanya. Walikuwa matajiri, na—na maskini walikuwa maskini. Nao wangeweza kuandaa hizo karamu kubwa. Loo, jamani, jinsi wangeweza kweli kuifanya ya kuvutia! Na, mwajua, ibilisi anapenda kuifanya dhambi ya kuvutia. Wewe... yeye... Hilo ndilo linaloifanya ya kuvutia sana.

83 Halafu basi, tunaona ya kwamba wangejitayarisha kwa miezi na miezi, na kutuma mialiko hii, nao wangeweka kila kitu tayari. Nao walichagua wakati fulani wa mwaka kwa ajili ya karamu kama hiyo, labda wakati zabibu za—zao zilipoiva na he—hewa ikajaa harufu nzuri ya zabibu hizo zilizoiva. Jamani, ingekufanya tu uwe na njaa ya kuvinusia, nao walijua jinsi ya kufanya kila kitu sawa kabisa.

84 Halafu wange—wangepamba ninii ya—yao, mnayoita hapa, nadhani, ukumbizo, ama baraza, tuliita huko kaskazini, na—na kuipamba vilivyo, na kuifanya ya kupendeza sana. Wangefanyia karamu hii kubwa huko nje barazani ambako kumezungushiwa ua, ili kwamba watu wa nje, na wale ambao hawakualikwa hawangeweza kuingia. Na, loo, jinsi wangebanika nyama ya mwana-kondoo na kuitia viungo vya kila namna! Na jamani, kweli wangeweza kuifanya ionekane nzuri, na ilikuwa nzuri.

85 Halafu wangefanya... wangeandaa kila kitu vizuri kabisa. Wangetengeneza mazizi yao yote kwa ajili ya wale waliokuja kwa mkokoteni, wapate kuwavuta farasi wao ndani. Walikuwa na maboma ya kufungia, watumishi pale, ambao mara tu... Watumishi wao wote, wote wamevalia kama watumishi, huku wamesimama tayari.

86 Ndipo wakati gari la farasi lilipokuja, wale waliosafiri kwa gari la farasi, wale watumishi wangelichukua hilo gari la farasi, washuke, wawaondoe farasi, na kuwaondolea lijamu na hatamu, na—na kuwapa chakula cha mifugo, na kadhalika, na kwa yule aliyepanda matandiko, waondoe hayo matandiko, na kumshughulikia farasi. Walikuwa wameandaa kila kitu.

87 Halafu basi, kulikuwako na mtumishi mwingine nimpendaye, mtumishi mwenye bei rahisi kuliko wote, na huyo alikuwa ni mtumishi mtawadha miguu. Alikuwa ndiye mtu anayelipwa kidogo kuliko wote katika kundi hilo.

88 Hilo ndilo linalomfanya kuwa Mungu kwangu mimi. Yeye alikuwa ndiye Mkuu wa wakuu kisha akachukua sehemu ya mtumishi mtawadha miguu duniani. Nasi tunatembea huku na huku, tukifikiri sisi ni mtu fulani. Naye Mungu wa Utukufu, huku akiufunua utukufu wa Mungu, alitawadha miguu ya wavuvi. Na hilo ndilo linalomfanya halisi, alifanyika Mtumishi, mtumishi duni kuliko wote, alipiga magoti Yake ili kutawadha miguu ya mavumbi yenyewe aliyoyaumba. Amina.

Huyo hapo, amepiga magoti akitawadha miguu, mtu anayepewa malipo duni kuliko wote katika hilo kundi, na kazi iliyo mbaya kuliko zote.

89 Sasa, watu walikuwa tu na karibu njia mbili za *kusafiria*, hizo zilikuwa ni ama kwa mnyama au kutembea. Basi watu walipotembea, walipanda juu ya vilima, njia za mkato, na kadhalika, juu ya vilima kwenda mijini. Na kwenye mkondo huu, wanyama pia walitembea, fa—farasi, na nga—ngamia, na punda, na barabarani walikoenda mavumbi yalikuwa yamechafuka.

90 Ndipo watu walipotembea, walikuwa wamevaa vazi la Kipalestina, ambalo ni joho, na ndipo walipokuwa wakitembea, vazi lilifika chini, nayo mavumbi, walipokuwa wakiitupa miguu yao, hilo joho lilibembea, nalo likaokota mavumbi barabarani, nayo yakaingia kwenye viungo vyao, nyusoni mwao. Nayo harufu ya kitalu, kama ninii. . . ambapo wanyama walikuwa barabarani ilikuwa juu yao.

91 Nao hawakuwa. . . wa—walijisikia vibaya kuingia nyumbani kuwa mgeni, wakiwa na harufu hiyo yote juu yao. Kwa hiyo kile wangefanya, wangekuwa na lundo kubwa la, kile ambacho tungekiita siku hizi, kama zile wanawake wanazovaa, maskini ndara za nyumbani, ndogo, kitu kama kipande kidogo cha nguo wanachovaa miguuni mwao. Ndipo basi wangeweka hizi zote katika safu ndogo.

92 Na labda mtu fulani anajitokeza, na hili hapa lililotukia. Njoo hapa, Ndugu Roy, kwa dakika moja. Hivi ndivyo walivyosalimiana. Walikuja namna *hii*, nao wangechukua kiatu chake, na kukivua, ndipo waone kiatu chake kilikuwa na ukubwa gani, kisha wakilinganishe na jozi ya—ya ndara za chumba cha kulala, tungekiita.

93 Na sasa, basi, wangeinama na kumtawadha miguu, na kuisafisha miguu yake vizuri sana, wachukue taulo, waipanguse vizuri, na kufikia kwenye viungo vyake. Ndipo basi inge—ingeondoa uvundo wote kutoka miguuni mwake, na mavumbi, na barabarani, nao wangemwondolea hayo yote. Ndipo angemvalisha maskini jozi ya—ya ndara hizi ambazo zingeienea vizuri miguu yake, basi wangezivuta miguuni mwake.

94 Ndipo angeenda kule, kungekuwako na mtumishi mwingine amesimama pale ambaye alichukua marhamu, mafuta, nayo yalikuwa yametiwa manukato sana, wangepata manukato

hayo kutoka kwa tofaa dogo linalotokana na ua la waridi linalotengeneza hayo manukato, nao wanatengeneza manukato haya na kuyamimina mikononi mwao, nao wangeipangusa mikono yao.

95 Halafu basi, usafiri katika siku hizo, mwali huo wa moja kwa moja wa jua hilo la Palestina ulikuwa mkali, ungeunguza shingo yao na uso wao. Ndipo wangechukua manukato haya na mafuta, na kupangusa uso wao, na juu ya masikio yao. Kisha angempa taulo, ndipo angeupangusa uso wake na kujiandaa.

96 Halafu basi, mnaona, alitawadhwa miguu yake, na kuvaa jozi ya ndara, alikuwa ameondolewa mavumbi. Na hiyo ilikuwa na namna fulani ya, kitu kama, manukato hayo yangetumika kama vile mentha ingekufanya ujisikie baridi na kuburudika. Akajiandaa, ndipo basi alikuwa tayari basi ku—kukutana na yule aliyekuwa amemwalika. Sasa, hakujisikia kukutana naye akiwa mchafu kabisa.

97 Natumaini ninyi watu mnapata mfanano wa huo, wa wakati tutakapoenda kukutana na Mungu. Mnaona? Haina budi kuoshwa, dhabihu, sikuzote, na ilikuwa imeandaliwa na tayari, imewekwa tayari. Na hivyo ndivyo tunavyofikia, mahali tunapoenda kukutana na Mungu. Hatuna budi kuja kwanza na kuoshwa kwa maji ya Neno, kweli, yaliyotiwa manukato kwa mafuta ya kutia yaliyoingia kwenye ndevu za Haruni, yaliyopita hata pindo za mavazi yake, upendano wa ndugu, kuingia katika mahali hapa Patakatifu, patakatifu.

98 Ndipo, alipoenda kwenye karamu iliyokuwa imemwalika, alipokuja mbele zake, sasa, vipi kama angeingia na miguu michafu, inayonuka na mavumbi mwilini mwake? Alinuka vibaya, ange—kidogo angejisikia vibaya. Angemkwepa. Lakini basi, baada ya kutawadhwa miguu yake, na kutiwa mafuta, kama vile tunavyotiwa mafuta na Roho Mtakatifu, mnaona, kisha akajiandaa kabisa, basi aliingia kwa bwana wa nyumba, mfawidhi wa sherehe, ndipo alikuwa—alikuwa tayari kukutana naye.

99 Na hivi ndivyo walivyofanya. Walishikana mikono, namna *hii*. Sasa, vipi kama alikuwa ananuka uvundo sana? Asingetaka kumkumbatia. Lakini, mnaona, amejiandaa sasa, yuko tayari kwa ajili yake. Kwa hiyo wakakumbatiana namna *hii*, na ndipo akawa amekaribishwa.

100 Sasa, huko kupeana mkono kwa mwisho (Asante.), huko kupeana mkono kwa mwisho kulimkaribisha. Lakini alikuwa na maandalizi kwanza, kabla hajapewa mkono huo na, mara nyingi, busu shingoni, alimkaribisha kwa busu, akamshika mkono, akamkumbatia, na kumbusu pande zote mbili za shingo, hiyo ilimaanisha alikaribishwa. Sasa, asingejisikia kumruhusu kumbusu akiwa na vumbi hilo lote na uvundo juu yake.

Mnaona? Lakini maandalizi hayo yamefanywa. Loo, jamani! Laiti tungeweza kulipata! Matayari-. . .

101 Mnakumbuka katika ule mfano, jinsi mtu mmoja alivyoingia bila vazi la arusi? Alikuwa amepitia mlangoni ama dhehebu fulani, hakuwa amepitia. . .alikuwa amepitia dirishani, si mlangoni, ama kama angalipitia mlangoni, angeninii, angepata joho. Alipitia njia ya kanuni fulani za imani ama dhehebu, alitupwa nje, hakustahili kuketi mezani.

102 Hana budi, kwanza hana budi kuoshwa, na kuandaliwa, na kutiwa mafuta, ndipo alikuwa tayari kuingia. Na wakati. . . Mradi tu yeye, akiwa ni mgeni, naye alikuwa amealikwa, na alikuwa. . .jambo la mwisho lilikuwa ni kumsalimia kwa mkono na "*kumbusu*" kumbusu shavuni, ama, shingoni, na hilo lilimkaribisha kwa busu.

103 Loo, yeye alikuwa ni ndugu kamili basi! Amina. Naam, alikuwa amekaribishwa basi. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .ingia kwenye friji na ujitwalie sambusa kubwa ya Dagwood, na kujilaza kitandani, uko nyumbani, unaona. Umekaribishwa, maadamu umepewa busu hilo la makaribisho, kama yule mwana mpotevu, mwajua, akirudi, maadamu umepata busu la makaribisho. Sasa, ilikuwa—ilikuwa ni sawa.

104 Kwa hiyo siku hii ilikuwa imewekwa, na kila kitu kilikuwa kimeandaliwa, na wana-kondoo wote walikuwa wamechinjwa, na—na kuchoma nyama kulikuwa kunaendelea, mwana-kondoo wa kubanikwa. Loo, jamani, hewa kote mjini, na chini bondeni ilikuwa tu. . .harufu nzuri ilikuwa tu imetandaa mahali pote, ikichanganyikana na divai, na zabibu, na kadhalika. Na di—divai iliyo bora sana waliyotumia, na kila kilicho bora sana, kwa sababu wangeweza kugharamia kilicho bora zaidi.

105 Basi walikuwa wameandaa kila kitu. Watumishi wote walikuwa wamesimama mahali pao, taulo mabegani, kila mtu mahali pake. Hiki hapa gari la farasi linakuja, na huyo mtumishi akaondoka naye, kisha akaingia, kutawadha miguu, na kadhalika, kuendelea na kuendelea na kuendelea. Ni siku ya jinsi gani! Maskini huyo Farisayo alikuwa na wakati mzuri sana!

106 Sasa, nitawaambia ujanja aliokuwa nao kisiri. Nitauchukua kutokana na dhana ya yale Biblia isemayo juu ya jamaa hao. Hawakuamini Yeye alikuwa ni nabii, hawangeweza kuamini, walimwita Beelzebuli, mpiga ramli. Wala wasingeweza kumwazia Mtu huyo kuwa ni nabii. Mnaona, huenda hamkuyawazia mambo haya hapo awali, lakini Maandiko yote yamejaa hayo. Mnaona? Jinsi tu unavyoliangalia. Angalieni, wala hawakuamini Yeye alikuwa ni nabii.

107 Kwa hiyo ningewazia maskini Farisayo alisema, "Sasa, nimemwalika Rabi *Nanii* na Rabi *Nanii*, nami sina budi kuwa na burudani kuu. Nami nitamleta mdanganyifu huyo hapa chini. Nanyi mnajua tutakalofanya? Nitamwonyesha, nitathibitisha

ya kwamba yeye si nabii. Rabi Belinski hapa, anaamini ya kwamba yeye ni ninii tu. . .yeye ni mwongo. Haamini, kwa sababu anayapinga sana madhehebu yetu. Kwa hiyo yeye—yeye ananinii tu. . .Hatuwezi kuamini. Kama angalikuwa ni nabii halisi angekuwa Mfarisayo na kuyatetea mambo tunayotetea."

108 Jamani, roho huyo wa kale hakufa kamwe! Yule mtu aliyempagaa alikufa. Lakini, mnaona, Mungu na ibilisi: Ibilisi humchukua mtu wake, bali roho wake anabaki, kweli, roho yule yule anabaki kote katika nyakati; naye Mungu humchukua mtu Wake, bali kamwe si roho Wake, anaendelea, pia.

109 Kwa hiyo imekuwa ni vita kote kote. Nawe huna budi kujichagulia, kwa hiyo, mojawapo: asiyeamini, na mwaminio. Naye asiyeamini sikuzote ana maringo, hujifanya kitu fulani, mwajua. Na—nasi tunaona ya kwamba wakati mwingine Mungu hufanya kazi kwa njia nyenyekevu sana, Yeye anawafumba tu macho jamaa hao.

110 Kwa hiyo basi, hawakuamini Yeye alikuwa ni nabii. Nami naweza kuwazia maskini Askofu Farisayo amesimama karibu, akisema, "Mwajua nini? Nitakapomleta hapa, nitamfanyia moja ya kutosha. Nami nitamwingiza humu ndani, nasi tutathibitisha ya kwamba yeye si nabii. Na, ho, ho, mnajua nini? Jamani, nawazia shirika langu litanifanya mzee wa wilaya wakati mwingine," ama kitu fulani, mwajua, limpe kitu fulani kikuu, maana kweli alimfunua Mtu huyu, mwajua. Yeye kwa kweli, hakuamini ya kwamba Yeye alikuwa ni nabii, kwa hiyo, a—akamleta kule chini.

111 Kwa hiyo wakati shirika lote lilipokutana, na hao wote, ninawazia walikuwa na wakati mzuri wa kupongezana, na kunywa, na kuwa na wakati mzuri, ungeweza kumsikia maskini huyo Farisayo akipiga makelele zaidi ya hao wote kule juu, mwajua, wakipiga makelele tu. Jamani, ni wakati wa jinsi gani waliokuwa nao, wakati mzuri sana!

112 Na sasa, hebu tuangalie pande zote kwa dakika moja. Aliingiaje mle ndani? Alipataje kupita lango la hao watumishi? Huyo hapo ameketi pembeni. Alifika kwa wakati mzuri kabisa; daima Yeye hachelewi. Naye huyo hapo ameketi pembeni, nachukia kusema jambo hili, ameketi pale akiwa na miguu michafu. Yesu, mwenye miguu michafu. Kama vile Mfaransa anavyomwita, "Jésus," Jésus, akiwa na miguu michafu. Hakuna mtu aliyekuwa amemwosha, hakuna mtu aliyekuwa amemwandaa, kumtia mafuta, na hata hivyo, alialikwa. Basi huyo hapo Yesu ameketi na miguu michafu, aliyekuja kwa mwaliko aliopewa, bali hakuna mtu aliyemjali. Alimpitaje huyo mtumishi mtawadha miguu?

113 Laiti ningalikuwa na kazi hiyo. Ningekuwa nikimtazamia, ningekuwa nikiangalia juu chini barabarani. Ningalihakikisha

Yeye alioshwa, kama ningalikuwako pale. Ningetaka kuhakikisha kwamba nimeitawadha miguu *Yake*.

114 Lakini huyo mtumishi alikuwa wapi? Mmoja alikuwa wapi? Bado alikuwa na uvundo wa barabarani, alikuwa na miguu michafu, hakutiwa mafuta, Maandiko yanasema hivyo, naye Huyo hapo ameketi pale, wala hakuna anayemjali.

115 Hivyo ndivyo ilivyo katika ninii yetu, miamsho mingi siku hizi. Ninachukia kusema jambo hili, bali ni kweli. Tunamwalika na kujaribu kumpuuza. Mtu fulani anaweza kusema jambo fulani, ama kuanza kumwabudu Mungu tunapomwomba Yeye aje, Naye huja katika mfano wa Roho Mtakatifu, ndipo mtu fulani atasema jambo fulani, naye ataninii . . . mtu fulani ataanza kuabudu, nalo litausumbua mkutano wote, kwa sababu mtu fulani alisema, "Amina," ama "Haleluya." Kumpuuza! Na kama mtu fulani angesema, mtu fulani aseme, "Amina," "Haleluya," wangesema "mtakatifu anayejibingirisha," ama jina fulani chafu. Jésus akiwa na miguu michafu.

116 Mungu, kizazi hiki cha watu kina shida gani? Wako wapi? Nini kimetukia? Jésus, akiwa na miguu michafu, ameketi miongoni mwa watu ambapo amealikwa na akiwa na jina chafu. Huyo hapo ameketi pale, akiwa na uvundo wa barabarani, kila kitu wanachoweza kumtupia, ama watu wanaoabudu, na kukitupa, wanawaita kundi la makabwela na chochote kile. Jésus, mwenye miguu michafu.

117 Lakini Yeye kamwe hakusema Neno, Yeye aliketi tu hapo ameinamisha kichwa chake, ua la ukutani, kama vile tungeliita, karamuni. Hivyo ndivyo alivyo siku hizi ibadani, kwenye ibada ambako tunapaswa kuwa tukiwakilisha Pentekoste, Yeye anakuwa ua la ukutani.

118 Hapa si muda mrefu uliopita, mwinjilisti mashuhuri alikuwa huko Shreveport, naye alikuwa akiendelea kuhubiri, naye ni mhubiri hodari pia, naye alikuwa akiendelea kuhubiri, basi ndugu mmoja Mpentekoste wa thamani alikuwa amezoea kumsifu Mungu, ndipo Roho Mtakatifu akamshukia, akasema kwa sauti kuu, "Utukufu kwa Mungu!"

Ndipo mwinjilisti huyu akageuka na kusema, "Funga kinywa chako. Unanisumbua."

119 Vema, mimi unanisumbua wakati husemi, "Utukufu kwa Mungu." Na—nafikiri jambo fulani limetukia.

120 Nilikuwa na maskini mbwa mmoja, maskini huyo jamaa, alinipeleka shuleni kwa kuwinda. Angekimbiza mtini chochote kilichokuwako, ila yeye . . . kitu kimoja alichoogopa, ama hakutaka kukifikia, kilikuwa ni kicheche. Naye angempata chini ya lundo la vichaka, naye ange—angezunguka-zunguka tu akibweka. Kama nilitaka amshike, aende na kweli amshike yule kicheche, jambo pekee nililopaswa kufanya lilikuwa ni

kumpigapiga, na kusema, “Mkamate, jamani!” Aliingia na kumkamata yule kicheche.

121 Kicheche mkubwa kuliko wote nimjuaye ni ibilisi. Njia bora kuliko zote nijuayo ya kufanya hivyo, ni kusema, “Amina. Haleluya!” Hiyo ni kusema, “Mkamate, jamani! Mfuate. Mweke kwenye kisiki.”

122 Naam, wanamwalika, bali hawamtaki. Anapokuja hawatampokea, wana njia yao wenyewe ya kidesturi, nao hawana budi kuwa nayo hivyo.

123 Hakaribishwi baada ya Yeye kufika kule, kila mtu anampita kana kwamba hakuwako, akiangalia huku na huku, akisikia mizaha ya kisasa ya Mafarisayo.

124 Kama baadhi ya mitindo hii ya televisheni tuliyo nayo siku hizi, watu afadhali wakae nyumbani na kumwangalia Ricky fulani akisimama, kule chini akiwa na mtindo wa televisheni na kufanya mzaha wa namna fulani, na mwanamke fulani ambaye ameolewa mara nne au tano, na kadhalika, na kukaa kusikia hayo, na kupenda hayo kuliko wanavyopenda mkutano wa maombi Jumatano usiku.

125 Mbona, si ajabu uamsho umekwisha! Huwezi kujenga Kanisa juu ya makaa au majivu, hadithi fulani ya kale. Huwezi kufanya hivyo. Makaa ya kale yaliyoteketea! Huna budi kuwa na mtu ambaye moyo wake unawaka moto, wanatazamia jambo fulani, jambo fulani kutukia, wakiangalia kila ibada, papo hapo mahali hapo, wakiangalia.

126 Tunamwalika na kumwita, halafu hatumtaki anapofika kule, tunampuuza tu, tunaachana Naye, hatumjali. Neno Lake linaweza kusomwa, ama kuhubiriwa, wanaketi tu na kuliacha lipite, labda ulale usingizi mzito unapofanya hivyo. Mnaona? Haliwavutii.

127 Kukesha, kutazamia Kuja kwa Bwana! Tumemwalika, tunamtaka, “Njoo, Bwana Yesu, njoo,” na hata hivyo hatuninii . . . tunaonekana kulipuuza wakati anapoingia miongoni mwetu.

128 Hapo, Yeye aliketi pale, hata hivyo, alikuja. Nashangaa ni kwa nini, nashangaa ni kwa nini; daima kuna sababu. Huko chini kabisa barabarani, kando ya barabara kuu, akaingia barabara ndogo, ya mavumbi, akashuka kichochoroni, chini kabisa uchochoroni, kisha akapanda vipandio vidogo *vinavyokereza* akiingia kwenye kibanda kidogo, ninamwona maskini mwanamke mmoja akitokea. Anaangalia kote, “Kwani kila mtu yuko wapi?” Anateremka kwenye vipandio vinavyokereza. Loo, ninaamini alikuwa ni maskini msichana mrembo. Naye akaja akishuka kwenye vipandio. Alikuwa amechukua njia mbaya, kweli, lakini labda, mwajua, huenda ilikuwa ni mzazi fulani aliyemwacha afanye hivyo.

129 Mwajua, mnazungumza sana, siku hizi, kuhusu kutowajibika kwa vijana, ninaamini ni kutowajibika kwa wazazi, ninaamini hapo ndipo lilipo. Nena kuhusu ujinga wa Kentucky. Acha mmoja wa hao wasichana huko juu aingie, usiku kucha, amelewa nusu, nayo rangi yake ya midomo, vyovyote mnavyoiita, kote usoni mwake, na ni nusu uchi, amejinengua namna *hiyo*, ndugu, mmoja wa maskini hao mama wa Kentucky angejikatia tawi kutoka kwenye mojawapo wa miti hiyo, naye atachakaza nguo alizo nazo, zimtoke. Kweli. Yuko mbali sana na Hollywood, mwajua. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo tunalohitaji leo hii, mama wengine wa aina *hiyo*. Hiyo ni kweli. Ndivyo hakika.

130 Ndipo tunaona ya kwamba anashuka kwenye vipandio, anaingia uchochoroni, anaangalia kila mahali, kuna . . . "Kwani yuko wapi kila mtu?" Mnaona, huyo mtoto alikuwa amefukuzwa, hakuna aliyemjali.

131 Hilo ndilo linalowafanya wasichana wengi kupotoka, kwa sababu inaonekana hakuna mtu anayemjali. Kungekuwako, nusu yao wasingekuwa jinsi walivyo, kama kuna mtu angeweza . . . angewajali. Badala ya mama na baba huko nje mahali fulani, wakipiga makelele katika baa na kumwacha msichana wao aende popote, wanapaswa kuwa nyumbani wakiomba, Biblia yao imefunguliwa, wakiwaombea, kama vile Ayubu alivyokuwa akiomba kwa ajili ya watoto wake, "Labda wanatenda dhambi," angetoa dhabihu kwa ajili yao. Tunahitaji maombi zaidi na nyumba zaidi zilizowekwa wakfu kwa Mungu. Hiyo ni kweli.

132 Sasa, labda wazazi wake walikuwa wahalifu walioenda kombo, wakamwacha aende. Maskini msichana huyo alijipatia riziki yake kwa maisha machafu, mnajua ninalomaanisha, na kwa hiyo, hiyo ndiyo njia aliyokuwa nayo ya—ya kujipatia riziki. Tunajua lilikuwa jambo baya sana, lakini hata hivyo, labda alikuwa . . . Nasi tutawazia ya kwamba alibadilika akawa hivyo, kwa sababu kulikuwa na wema fulani nyuma ya mwanamke huyo, ilithibitika hivyo. Kweli. Kitu fulani huko nyuma kilikuwa halisi. Ndipo ninaamini Yesu alijua hivyo wakati yule Farisayo alipomwalika, hakika, Yeye alikuwa akiiendea nafsi hiyo.

133 Ndipo tunaona, ya kwamba anaingia kisiri kwenye barabara hiyo nyingine, anaangalia huku na huku, macho yake makubwa mazuri *yanametameta* kote, "Mbona, kwani kila mtu yuko wapi?" Anashuka kupitia mitaani, yote ni tupu.

134 Sasa, maskini wasingeweza kuja kwenye karamu hizi, lakini mwajua, wangekuja uani, "*kunusa*," wangesikia harufu hiyo, nayo matumbo yao yangenguruma tu, walitaka kuninii . . . kitu cha kula sana, bali wasingeweza kuingia, matajiri hawa walikuwa nacho, nao wakakiweka. Kilikuwa tu ni kwa ajili ya matajiri.

135 Kwa hiyo akaangalia kote, akashuka, "*akanusia*," moja kwa moja akasikia harufu fulani. Maskini tumbo lake tupu likaanza kulilia kitu fulani, mwajua, "Mmmm! '*Nusia*,' mmmm! Loo, hiyo ni kweli! Ninakumbuka kwenye tangazo, yule Askofu Farisayo *huko* juu anafanya mkutano wake mkuu wa kila mwaka. Vema, nadhani sitakuwa na kitu cha kufanya leo, ila kutembea huku na huku." Sasa, alikuwa ametengwa na mtu yeyote, mwajua. Kwa hiyo yeye . . .

136 Sasa, hebu tumwangalie. Anajipenyeza karibu. Naye ilimbidi awe mwangalifu asije akakaribia mahali walipokuwa watu wengine, wangemwona, maana wangechukua jiwe na kumfukuza. Kwa hiyo, wingi wa huo Ufarisayo wa kujifanya unaendelea siku hizi, pia. Hiyo ni kweli. Wanahitaji kunyooshewa mkono, kumbuka ulikotoka pia, unaona, kabla hujamtupia mtu mwingine jiwe, unaona.

137 Sasa, hapo ninamwona wakati akitembea kuelekea langoni. Maskini jamaa huyo alikuwa na njaa, "*nusa*," angeweza kunusa harufu ya huyo mwana-kondoo aliyechomwa, na, loo, jinsi ambavyo angetaka kumla! Basi akarudi nyuma ya huo umati, akitembea, angeweza kukinusa, naye, "*nusa*," angalau angeweza kufurahia kunusa harufu nzuri huku hewa ikiipeperusha kutoka kwenye mashimo makubwa ya jiko la nyama choma mle ndani. Naye angeweza kumsikia Mfarisayo juu ya hao wote, "Ho, ho, ho, ho, ho! Askofu, ninataka kukuuliza jambo fulani hapa. Daktari, njoo huku," mwajua.

138 Na kwa hiyo, akawasikiliza kwa dakika chache. Naye akaendelea mbele kidogo, akasimama mahali padogo, juu kidogo, kusudi aweze kuona juu ya vichwa vyao. Akaanza kuangalia huku na huko barazani, naye akawaona wageni wote, jinsi walivyokuwa wameandaliwa na ni nadhifu, na jinsi nguo zao zilivyo ninii tu, ninii moja . . . naye kuhani, akiwa na majoho yake yote ya kufuma lesi na kila kitu, amesimama karibu, jinsi walivyokuwa wa ajabu.

139 Basi angalieni, huku wakizungukazunguka pale, maskini watoto wadogo wenye njaa wakining'inia uani, wakilia wapate chakula. Mwangalie maskini mama dhaifu amesimama pale, amemshika mtoto mchanga, huku midomo yake ikitetemeka, akishikwa na hamu sana apate chakula, nao mle ndani, wakiendelea jinsi walivyokuwa wakiendelea.

140 Na, mwajua, mara, macho yake yakaona Kitu. Kuna jambo fulani kumhusu Yeye, sijui, kama macho yako yakipata kumwona kidogo, unajua hilo, hiyo ni kusema, kama umekusudiwa Uzima. Naam. Vinginevyo, unaweza kumwangalia moja kwa moja wala haikuvutii. Lakini kama umekusudiwa Uzima, mtazamo wa kwanza, Yeye ni tofauti.

141 Akaangalia, akasema, "Maskini Jamaa yule, anayeketi pale, mwajua, kuna jambo fulani kumhusu ambalo—ambalo ni

tofauti. Kuna nini kuhusu Mtu huyo? Yeye ni nani, nashangaa? Mbona, Yeye hata hajaoshwa! Aliingiaje mle ndani? Ilibidi aalikwe, la sivyo asingeweza kuja. Naye Huyo hapo, ameketi pale, wala hajakaribishwa, miguu Yake ni michafu. Pia angalia, kila mtu ananinii tu. . . " Wanafunzi wake wasingeweza kuja, hawakualikwa, iliwabidi kukaa nje.

142 Anasonga mbele, nami ninamsikiliza. Anasikia mazungumzo, na ilikuwa ni mmoja wa wanafunzi, kasema, "Nashangaa ni kwa nini hawajamtayarisha Bwana wetu. Huyo hapo ameketi pale."

143 Ndipo akaanza kuweka mbili na mbili pamoja, "Huyo hana budi kuwa ni *yule* Nabii. Hapana shaka huyo Ndiye waliyemkokota mwanamke yule wa aina yangu mbele Zake, nao wakamwomba, kumpiga Yeye mawe afe, ama, kumpiga mawe mwanamke huyo hata afe. Naye akasema, 'Wa kwanza asiye na dhambi, tupa jiwe la kwanza.' Loo, hii ndiyo nafasi yangu!" Ni tofauti jinsi gani na yule tarishi wa kuajiriwa! "Hii ndiyo nafasi yangu, Huyo hapo, laiti ningaliweza tu kumfikia! Lakini Yeye amefungiwa na uzio kutoka kwangu."

144 Kuna mioyo mingi yenye njaa katika Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Katoliki, na kadhalika, wamefungiwa mbali Naye kwa kanuni za imani. "Laiti ningaliweza tu kumfikia Yeye!"

145 Naye akaangalia, naye akamwona, akasema, "Anahitaji kuhudumiwa, anahitaji kushughulikiwa, nami lazima nifanye hivyo." Kwa hiyo akawazia juu ya. . . Kitu fulani kikamgusa moyoni, huyo akageuka, akashuka barabarani, akashukia uchochoroni, kwenye maskini vipandio hivyo vinavyokereza tena, akafungua komeo la mlangoni, akaingia ndani, akaunyoosha mkono chini ya kitanda, akatoa kibweta chake cha ninii yake. . . vitu vidogo alivyovijali. Akanyosha mkono kwenye kona, juu ya soksi yake zilikuwa pale, akazitoa, akahesabu vipande thelathini vya dinari za Kirumi, kwa hiyo akasema, "Jambo ndilo hilo. Nitafanya hivyo." Basi akakifunga kile kibweta tena. Kisha kasema, "Loo, siwezi, siwezi kufanya hivyo! Yeye ni Nabii, Yeye atajua hasa mahali nilipopata hizo pesa na jinsi nilivyozipata, siwezi kufanya hivyo." Akaanza kuzirudisha kwenye hicho kibweta.

Lakini Kitu fulani kinasema, "Anahitaji kuhudumiwa."

146 Jambo ndilo hilo. Haleluya! Haidhuru wewe ni nini, Yeye anahitaji kuhudumiwa. Ndipo akachukua soksi yake tena, na, "Lazima nifanye hivyo!" Kulikuwa na kitu ndani yake, "Lazima nimfikie!"

147 Huyo akashuka kwenye maskini hivyo vipandio vilivyokereza, huku ameshika zile—zile pesa katika vazi lake. Naye akashuka mtaani ambako mmoja wa jamaa hawa alikuwa, mwajua, ya kwamba "hakuna faida ya kumwacha Yusufu shimoni," naye alikuwa anaenda kukaa na kuweka

biashara yake wazi, kama jambo lolote kweli lilitukia, mwajua, mtu fulani akaja karibu. Kwa hiyo anaingia, naye anasimama, mwajua, kama baadhi ya wafanyabiashara wa siku hizo, "Vema, unataka nini?" Mwajua, alipoona alikuwa ni nani. "Unataka nini humu ndani, kwa vyovyote vile?"

"Ninataka kibweta cha marumaru yaliyo bora kuliko yote uliyo nayo. Nataka yaliyo bora kuliko yote."

148 Loo, hilo ndilo! Mungu anakutarajia umpe chako kilicho bora kuliko vyote, si tu muda mfupi pembeni, bali anataka yaliyo bora kuliko yote, Yeye hana budi kupata yaliyo bora kuliko yote.

Naye huenda, akasema, "Unataka nini na haya?"

"Loo, ni kwa ajili ya tukio maalum! Lazima niyapate."

"Vema, kila mtu ameenda . . . "

149 Naye anamwaga hizo pesa juu ya—ya kaunta. Loo, bila shaka, kama kuna pesa ndani yake, hilo ni sawa. Akasimama, huyu hapa anakuja, akatoka, akahesabu, "Naam, kiasi sahihi kabisa cha dinari ya Kirumi. Hiyo ni kweli." Akaunyosha mkono na kuchukua kibweta kilicho bora zaidi cha marumaru. Naye akakiweka kifuani mwake, kisha huyo akatoka nje ya mlango.

150 Naye huyo karibu na ua, akasema, "Siwezi kuingia hapa ndani, mimi . . . Si—siwezi kujipenyeza kupitia pale. Sijui jinsi nitakavyofika kule, bali anahitaji kuhudumiwa, nami nitafika pale kwa njia fulani." Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. "Ninaenda kwa vyovyote vile, sijali mtu yeyote anasema nini, sina budi kumwendea." Jambo ndilo hilo. "Sina budi kufika pale."

151 Akashikilia hiki kibweta, na hiyo ndiyo riziki yote aliyokuwa nayo, hiyo tu ndiyo aliyokuwa nayo . . . katika ulimwengu huu kulikuwa na kile kibweta kidogo cha dinari, ambayo yeye, kile kibweta alichokuwa amenunua kwa pesa alizopata kwa njia mbaya. Na ilikuwa ni mbaya, alichukia kumwendea namna hiyo, bali hicho tu ndicho alichokuwa nacho, na hivyo ndivyo tu angaliweza kuja.

152 Hivyo ndivyo tu unavyoweza kuja, na hivyo ndivyo tu ninavyoweza kuja. Lakini anatutarajia kuja kama anahitaji kupendwa, kuhudumiwa. Anatutarajia.

153 Naye huyo hapo ameketi pale, ilionekana tu kana kwamba alikuwa akimngojea, akiangalia pande zote. Sijui jinsi alivyoingia, hata si—siwezi kuwazia jinsi alivyoingia, lakini aliingia, hilo ndilo jambo muhimu.

154 Sijui jinsi nilivyoingia, lakini nilifika kule. Amina. Hilo tu ndilo ninalojali. Ni—nilifika, nikafika kule, hilo ndilo jambo muhimu. Siwezi kuona jinsi angeweza kuingiza kitu kama mimi, lakini Yeye . . . kwa njia fulani, nilifika pale. Nilifika siku moja, daima nimebaki kule; kamwe sitaki kuondoka, niache tu nikae papa hapa.

155 Kwa hiyo akaingia mle. Alikuwa nalo mahali fulani moyoni mwake, kwamba . . . Sasa, alipofika pale, ilitokea aliwazia, "Vipi kama Yeye akigeuka na kunishambulia vikali? Vema, nitafanya nini?" Lakini kumbuka tu, unapojaribu kumtumikia Yesu, Yeye kamwe hatakukemea kwa kufanya hivyo. Huenda ukalipata kanisani mwako, bali hutalipata kutoka kwa Yesu. Hiyo ni kweli. Naam. Huenda ukakemewa na jitu fulani la kikanisa ambalo lingesimama na kusema, "Siku za miujiza zimepita. Komesha ushuhuda huo," na kadhalika, "kuhusu uponyaji huu wa Kiungu, upuuzi huu wa Roho Mtakatifu, achana na huo." Huenda ukalipata kutoka kwake, bali kamwe si kwa Yesu. La.

156 Hivi mliona, alijipenyeza nyuma Yake? Sasa, katika siku hizo, hawakula kama tunavyokula siku hizi, kuketi mezani namna *hii*, (*Hao* watoto wana fununu.), walijilaza chini kula. Walikuwa na kochi, nao wangelisukuma hilo kochi juu (Hakika, *hao* watoto wanajua wanalofanya, hakika wanajua.), na kwa hiyo, walilisukuma hilo kochi moja kwa moja kuizunguka meza, nao wakalala chini, nayo miguu yao imening'inia, nao wanakula namna *hii*. Wangali wanafanya hivyo huko mashariki, nimekula namna hiyo, mnaona, kulala chini namna hiyo. Loo, ni jambo zuri, mnapaswa kulijaribu wakati mmoja. Kwa nini msiseme, "Amina," wengine? Kwa hiyo basi, hiyo ndiyo njia.

157 Nao . . . Akaingia kisiri nyuma Yake, naye akawazia, "Mimi hapa, nami sasa nimewasili Uweponi mwa Uzima wa Milele. Laiti ningaliweza tu kumtumikia Yeye! Laiti ningaliweza tu kumfanyia jambo fulani!" Sasa, ilimbidi kwa namna fulani kuinamisha kichwa chake, kwa sababu alikuwa ni mwanamke aliyedharauliwa. Naye akapiga magoti, ninaweza kumwona akipiga magoti kando ya miguu Yake, naye akawaza, "Naweza kumgusa?"

158 Loo, ni—ni . . . Unaweza kuwazia jinsi alivyojisikia? Natumaini nitapata nafasi hiyo siku moja.

159 Kama vile mzee mmoja mweusi miaka mingi iliyopita, alikuwa huko chini kusini, alikuwa ameokoka, basi a—akazunguka akiwaambia ndugu wote kwenye shamba hilo alikuwa—alikuwa huru. Bosi akamwita ndani, kasema, "Mose, nataka kukuuliza jambo fulani. Nasikia unasema miongoni mwa watumwa kwamba uko huru."

Akasema, "Naam, Bwana." Akasema, "Niko huru." Kasema, "Jana jioni, Yesu Kristo aliniweka huru kutoka kwa adhabu ya mauti na dhambi."

Akasema, "Unamaanisha hivyo, Mose?"

Akasema, "Naam."

160 Akasema, "Basi nitashuka niende na kutia sahihi lile tangazo la kuwekwa huru, nawe unaweza kuwa huru kuwahubiria ndugu zako. Mimi pia ninakuweka huru, ikiwa Kristo alikuweka huru." Kwa hiyo akashuka na kulitia sahihi.

161 Huyo mzee akahubiri kwa miaka na miaka. Alipofikia wakati wa kufa, wengi wa ndugu zake wazungu aliokuwa amewahubiria walikuja. Alikuwa amelala huku amepoteza fahamu, nao walidhani alikuwa ameaga, alilala pale labda siku moja au zaidi bila kuzungumza.

162 Siku moja, akafumbua macho yake, akasema, "Kwani ningali hapa? Kwani ningali hapa?" Akasema, "Njoni karibu, ndugu zangu." Akasema, "Nilifikiri nilikuwa nimevuka Upande ule mwingine, nami ndio kwanza niingie tu kupitia langoni, yule Malaika Mkuu alikuwa ameniruhusu kuingia langoni." Kisha kasema, "Hawa hapa watumishi fulani wakaja na kusema, 'Mose, Mose, mtumishi wa Bwana! Hili *hapa* joho lako, hii *hapa* taji yako.'"

Akasema, "Nikawageukia na kusema, 'Loo, watumishi wa Mungu, msinizungumzie kuhusu joho na taji.'"

Kasema, "Lakini, Mose, ni thawabu yako."

Akasema, "Sitaki joho na taji, kwa thawabu yangu hebu nisimame tu nimtazame Yeye." Jambo ndilo hilo.

163 Nafikiri hivyo ndivyo sote tunavyojisikia, "Hebu nimtazame tu Yeye." Mara nyingi nimewazia, kama ni . . . nitakapovuka kule, kama ningeweza tu kutambaa huko, na kuipigapiga miguu hiyo kidogo tu, niangalie mahali hilo kovu la msumari lilipokuwa, kisha nirudi nyuma, lingenilipa kama ningeishi miaka mia moja, na kuhubiri kila usiku, na kufanya kila nilichoweza, naam, kupigapiga tu miguu Yake.

164 Naye hapa mwanamke huyu alikuwa, miguuni Pake. Ni mahali pa jinsi gani kuwa! Na miguuni Pake akazikumbuka dhambi zake zote. Kuna jambo fulani kulihusu, unakumbuka kila jambo ovu ulilofanya unaposimama miguuni Pake. Naye alipofanya hivyo, aliwazia, "Mimi, mwovu kuliko wote, huku nimesimama hapa karibu na Patakatifu pa patakatifu!" Machozi makubwa mno yakaanza kutiririka mashavuni mwake, nayo yakaanza kudondokea miguuni Mwake, akageuka na kuanza kumwangalia.

165 Naye akajaribu kuiosha, ha—hangeweza, machozi yaliidondokea. Asingeweza kamwe kuitawadha miguu Yake ama kukivunja kile kibweta, naye angejaribu, nayo machozi, ndipo kwa namna fulani akaona aibu, yeye mwenyewe, akililia miguuni Pake. Naye a—akachukua . . . Nywele zake zikaanguka chini alipokuwa . . . mwajua, alikuwa amekunja mawimbi yake namna *hii*, mwajua, juu ya kichwa chake, na wakati yeye . . . machozi yake yakianguka miguuni Mwake, nazo nywele zake zikaanguka chini, akaanza ku—kupangusa machozi miguuni Mwake kwa—kwa mawimbi ya nywele zake. Baadhi ya dada zetu inawabidi kusimama kwa vichwa vyao wapate nywele za kutosha kufanya hivyo. Kwa hiyo basi, alikuwa akipangusa ninii . . . Miguu Ya—Yake kwa ninii—kwa nywele zake za kichwa

chake, huku yakidondokea mi—mi—miguu Yake namna *hiyo*. Na, loo, angeangalia juu, naye aliogopa! Na—naye . . . Wewe—wewe . . . mimi . . .

166 Kwa njia moja au nyingine unasisimkwa sana unapomkaribia, mimi husisimkwa. Ninasisimkwa sana ninapomhisi karibu nami. Wakati mwingine sijui ninachofanya wakati ninaponinii . . . Mimi—mimi hujipoteza, nafikiri sote hufanya hivyo.

167 Naye alipokuwa akijaribu kusema jambo fulani wala asingeweza, machozi yakitiririka tu miguuni Mwake. Hakuwa na maji yoyote ya kuitawadha miguu Yake, wala Farisayo hakuwa amempa maji. Lakini jinsi alivyokuwa na maji mazuri! Machozi ya toba, yakiiosha miguu michafu ya Yesu. Loo, Mungu! Machozi ya toba, yakiiosha miguu michafu ya Jésus. Angeiosha, kisha *angeibusu*, na kuiosha, na—naye akavunja sehemu ya juu ya maskini hiki kibweta, ndipo akamimina marhamu pale, kisha akaangalia juu.

168 Sasa, kama Yeye angalijongea, mwanamke huyo angeondoka hapo katika dakika moja. Lakini Yeye alininii tu, kama alitaka kumtumikia, Yeye aliketi tu kimya na kumwacha afanye hivyo. Ninapenda hilo. Ukitaka kumtumikia, ninii tu . . . Yeye atakaa kimya na kukuacha uendelee na kufanya hivyo. Unaona? Kamwe hakumkemea, hakusema kamwe, "Aisee, ewe mwenye dhambi, simama uondoke hapo!" La, la. Alimwacha tu aendelee na kufanya hivyo. Atakuacha ufanye jambo lilo hilo kama unataka kumtumikia.

169 Na wakati machozi, na ninii . . . naye akichukua nywele zake na kuitawadha miguu Yake, alikuwa tayari amesahau kuhusu maskini Farisayo aliyekuwa amesimama pale juu na hao wengine wote, alikuwa akimtumikia Jésus.

170 Hivyo ndivyo ilivyo, unasahau yote kuhusu maaskofu na mambo haya mengine yote, wakati wowote unapomtumikia Jésus, endelea tu kulitekeleza. Sijali mtu yeyote anasema nini, u—umeshika kazi kabisa, unafanya jambo fulani.

171 Naye alikuwa akiibusu miguu Yake, na "*busu*, *busu*" akiipangusa miguu Yake, na kujaribu kuweka marhamu hii pale, na machozi, na marhamu yakipitia miguuni Mwake.

172 Na hapo, muda si muda mwajua, ilitokea Mfarisayo aliangalia nyuma na kuliona. Loo, jamani! Alifura kama chura aliyepigwa risasi. Yeye, akaangalia juu, "Hmm, jamani!" Alitaka ndugu wote waone jambo hilo, mwajua. "Angalieni pale!" Naye akasema moyoni mwake, "Kama mtu huyu angekuwa ni nabii, angejua huyo alikuwa ni mwanamke wa aina gani. Kama angekuwa ni nabii, angemjua mwanamke wa namna hii, kile alichokuwa. Jambo ambalo linathibitisha, ndugu, yeye si nabii."

173 Lakini Jésus kamwe hakusema jambo, Yeye aliliangalia tu, aliendelea tu kumwangalia, naye alikuwa akifanya huduma

aliyopaswa kufanya. Kwa hiyo yeye . . . Aliendelea tu kuangalia. Na baada ya kitambo kidogo, alipomaliza, mwajua, basi aliogopa wakati huo, akaogopa, baada ya kuipangusa miguu Yake kwa nywele zake na, hapa, mdomo wake umejaa mafuta kutokana na hayo, nawazia alikuwa amechafuka.

174 Mnajua, *kwa njia moja au nyingine*, u—unaingia katika mchafuko unapo—unapoinama mbele za Kristo. Hiyo ndiyo shida ya watu siku hizi, wanajaribu kukwepa kuzaliwa upya. Mwajua, kuzaliwa kwokwote ni mchafuko, sijali kama kuko kwenye zizi la nguruwe, ama kama kuko katika chumba cha waridi, kilichopambwa, cha hospitalini, kuzaliwa kwokwote ni mchafuko.

175 Nako kuzaliwa upya ni jambo lile lile, ni mchafuko; bali Uhai unatoka kwenye mchafuko huo. Njia pekee unayoweza kupokea Uzima, ni kwa kuzaliwa, ni mchafuko, bali huleta Uzima. Watu wanajaribu kulikwepa, hawataki kuosha rangi ya makucha kutoka usoni mwao, baadhi yao, ama, mnakiitaje kitu hicho? Si rangi ya makucha. [Mtu fulani anasema, "Wanja."—Mh.] Wanja, huo ndio. Chochote kile . . . Sijui upuuzi huo wa kichaa. Unaonekana mrembo zaidi kama hungejipaka huo, na . . . Naam. Kama utajaribu kidogo Matendo 2 na 4, itashinda zote ambazo Max Factor ingeweza kutengeneza, nitawaambia hilo. Kama utajaribu tu kidogo ya hayo, itakuwa ni uzuri wa Milele, roho m—mtamu, mpole, mtulivu.

176 Hicho ndicho mwanamke huyu alichokuwa nacho. Hicho ndicho Esta alichokuwa nacho alipokuja mbele ya mfalme, hiyo ndiyo sababu aliwashinda wasichana wengine, kwa sababu alikuja amejivika roho mtamu mbele zake.

177 Sasa, huyu hapa mwanamke huyu mbele za Jésus, akiitawadha miguu Yake. Basi baada ya kumaliza ibada, aliwazia, "Atasema nini?" Akasimama, macho yake makubwa meusi, nayo michirizi ya machozi inadondoka, na mchafuko kote usoni mwake ambapo alikuwa ameibusu miguu Yake, naye akaangalia aone kile Yeye angesema.

178 Farisayo akisimama pale, kila mtu ametulia basi, hakuna mtu aliyekuwa akisema jambo, mwajua, walikuwa, kila mtu, wamekata pumzi. Ninaweza kumwona Farisayo akiwa na hasira ya haki, mwajua, ikimpanda. Loo, alighadhabika! Akawaza, "Kuwaaibisha watumishi wangu!"

179 Wangali wanawazia jambo lile lile wanapoona mchafuko kama huo, mwajua. Je, hiyo ni aibu? Ni heshima kwa kanisa lolote litakalomwona mtoto mchanga aliyezaliwa upya akitokea.

"Loo, ni aibu jinsi gani! Uaskofu wangu utaangamia." Hapo akasimama amefura tu kama chura. Ndipo akasimama hapo, wote . . .

180 Yesu alikuwa akimwangalia huyo mwanamke. Kwa hiyo baada ya kitambo kidogo, akageuza macho Yake. Tutaona kama

Yeye alikuwa ni nabii ama siye. Loo, jamani! Mnaona kile alichosema! Alisema, "Simoni, nina jambo la kukwambia." Huyu hapa anakuja! Tutaona kama Yeye ni nabii ama siye.

181 Akasema, "Ulinialika huku chini, nami nikaacha ratiba Yangu. Niliwaacha wagonjwa wamelala karibu na malango, niliwaacha wenye ukoma wakilia, niliacha umati wa watu ukinitafuta nyikani, na kuzunguka kingo za bahari wakijaribu kunitafuta, kwa sababu ulinialika, nami nikaja.

182 "Na nilipoingia mlangoni, kamwe hukuiosha miguu Yangu. Uliniacha niingie hapa ndani upate kuniaibisha, kunianika mbele za watu. Kamwe hukunipa upako, kuipaka mikono Yangu mafuta na uso Wangu unaowaka moto, kwamba nilitembea kwenye jua kuja kwenye mwaliko wako, kamwe hukufanya hivyo. Hukunikaribisha kwa busu. Uliniacha tu nije kama mdoezi.

183 "Lakini mwanamke huyu. . . " Loo, jamani! Atasema nini? "Lakini mwanamke huyu, ameitawadha miguu Yangu kwa machozi yake." Haleluya! "Wala hajaacha kuibusu miguu Yangu tangu amekuwa hapa." Jambo ndilo hilo. "Nami ninamwambia," (Loo, Yeye atasema nini?) "dhambi zako, ambazo zilikuwa nyingi, zimesamehewa zote." Jambo ndilo hilo. "Dhambi zako, ambazo zilikuwa nyingi, umesamehewa zote."

184 Loo, Mungu, jalia hilo liwe ndilo ombi langu! Jalia huyo awe ni mimi nitakapofika mwisho wa safari, jalia nimsikie akisema, kwa kila huduma ninayoweza kumfanyia, kila misheni ninayoweza kwenda, kila mahali ninapoweza kuhubiri, kila mwenye dhambi ninayeweza kumvuta, ninatumaini kumsikia akisema, "Dhambi zako, ambazo ni nyingi, zote zimesamehewa. Ingia katika Milki ya Uzima, katika. . .ambayo imeandaliwa kwa ajili yako, baraka hizi ambazo zimetayarishwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu." Nina hakika sote tunajisikia hivyo, sivyo? Sivyo?

185 Na tuinamishe vichwa vyetu, kwa dakika moja, tunapowazia juu ya mambo haya hapa. Hatutaki wakati wetu utuondokee.

186 "Dhambi zako ambazo zilikuwa nyingi. . . " Macho hayo yalikuwa na milia, uso huo umechafuka kabisa, lakini siku zake zote za sifa mbaya zilikuwa zimepita. Uovu wote aliowahi kufanya, ulikuwa umekoma basi, alikuwa anaingia Uzimani. Sijui, usiku wa leo, ni wangapi katika jengo hili wanaomthamini Yesu Kristo vya kutosha, hata mngetaka kumtumikia? Huduma bora zaidi ungeweza kufanya ungefanya tu kama yule mwanamke alivyofanya.

187 Njoni huku juu, karibu na madhabahu kwa dakika moja. Tumekuwa na uponyaji wa mwili kwa siku chache usiku, hebu na tupate uponyaji wa nafsi. Mbona usije usiku wa leo, na kusema, "Nitashika njia yangu pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Nitaondoka hapa usiku wa leo, na

kuishi maisha ambayo yataosha uchafu kutoka kwa miguu Yake. Nitaishi maisha ya utakatifu sana, mpaka wote nitakaokutana nao watajua ya kwamba nimekutana na Kristo. Nitashika njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa"?

188 Je, ungetaka kumtumikia? Kama ndivyo, si uje hapa juu sasa na kusimama madhabahuni kwa dakika moja, kabla hatujaendelea mbele katika ibada? Simama tu hapa, na kusema, "Ninataka ku—nataka kuweka mahali pangu huko nje kumtumikia Yesu. Ninataka kuja madhabahuni usiku wa leo na kuungama dhambi zangu zote."

189 Ninawazia juu ya maskini mwanamke mmoja, mlemavu, akilia huku amefunika macho yake kwa leso yake, ndugu Myunani akimleta huku chini.

Mvulana mdogo, akitembea hapa. Njoo, mwanangu, usijali. Njoo hapa, mpenzi, Mungu anakupenda. Yesu anakupenda, kijana mpenzi. Simama papa hapa.

190 Bwana Yesu, umrehemu huyu mvulana mdogo, Bwana, maskini macho yake mororo, ninaomba ya kwamba utaangalia chini moyoni mwake, Bwana, na kuosha kila dhambi.

191 Mwanamke huyu wa thamani, mwenye mvi, umri umempitia, naye anakuja sasa na machozi yake, Bwana. Yeye anakupenda na anataka kukutumikia. Lijalie, Bwana, anapofanya hivyo sasa. Yafute machozi yake kwa msamaha Wako, Bwana, na umpe kile anachotafuta.

Mtu mwingine aende zake.

Mungu abariki . . . huyu hapa mtu mwingine anakuja. Mungu akubariki, Bwana. Mungu, osha kila dhambi.

Simama papa hapa kwa dakika moja Dada, hebu na asimame.

192 Baba wa Mbinguni, mtu huyu huenda asiwe na maana kwa ulimwengu, huenda ikawa ni mfanyakazi tu anayefanya kazi kwa bidii, mtu wa kawaida tu anayesimama hapa, labda, kama Rais au mtu fulani angekuja mjini, hata wasingejua hilo, lakini Yesu amekuja naye akamtambua. Mungu, samehe kila dhambi, mpe, usiku wa leo, Roho Mtakatifu mbarikiwa, maji ya Uzima anaposimama hapa akingojea kwa unyenyekevu. Tujalie, Bwana.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia ninii changu kinyenekevu . . .

Ombeni sasa. Kila mtu, mwulize tu Mungu, "Naweza kukutumikia?"

Unapozuru wengine,

Yeye ameshuka mjini mwenu juma hili, akawapa uamsho, akathibitisha Yeye yupo hapa miongoni mwenu. Hivi hamtakuja?

Mwokozi, . . .

Mungu awabariki. Hilo linahitaji ujasiri kufanya hivyo.

193 Baba wa Mbinguni, mpe ndugu yangu wo—wokovu wa nafsi yake, Bwana. Jalia kila dhambi ioshwe na Damu ya thamani ya Bwana Yesu. Amekuja, Bwana, akiamini, Anataka kumtumikia Mungu. Una mahali kwa ajili yake, Baba, mweke katika Ufalme Wako usiku wa leo, na umpe Roho Mtakatifu anapongojea kusikia jibu Lako likirudi kutoka Mbinguni. Ninaomba, katika Jina la Yesu.

194 Mtu mwingine, jitokeze tu moja kwa moja sasa. Mtu huyu aliyesimama hapa, machozi yakitiririka kutoka machoni mwake, mkono mkubwa mno unaoparuza umeushika wangu, anamaanisha hilo, kwa uaminifu sana, Yeye anamaanisha hilo. Kwamba anapita kutoka mautini kuingia Uzimani sasa hivi.

Huyu hapa mwanamke wa thamani, mwingine, mwingine; Mwanamke Mhispania akija, Mungu akubariki, dada.

195 Baba wa Mbinguni, mbariki huyu dada yetu. Jalia amtumikie Yesu wa Nazareti usiku wa leo, kwa maisha yake, aoshe aibu yote kutoka kwenye Jina hilo la thamani la Bwana Yesu. Tujalie, Bwana.

196 Maskini mwanamke huyu, aliyeinama mabegani mwake, kazi ngumu ya siku imepitia hapa, na labda maskini mikono hii dhaifu imeyafuta machozi kutoka kwenye mashavu mengi ya watoto wachanga wanaolia. Usiku wa leo, Bwana, kuna Mkono mmoja unaoweza kuondolea mbali machozi yake kwa msamaha, huo ni Mkono ulioupiga-piga ule wa yule mwanamke, na kusema, "Dhambi zako, ambazo ni nyingi, umesamehewa zote." Mbariki, Bwana. Mjalie hili, kupitia Jina la Yesu.

Mungu, mwingine anayesimama, akiyapangusa machozi kutoka machoni mwake, mpe, Bwana, Uzima wa Milele kupitia Jina la Yesu Kristo.

Mwingine, Bwana. Roho Mtakatifu na awe juu yake. Ameuona Uwepo Wako, ninaomba ya kwamba utambariki sasa . . .?. . . Endeleeni tu . . .?. . .

197 Baba wa Mbinguni, ninaweka mikono juu ya hawa, wanawake hawa hapa. Wanataka kumtumikia Yesu. Tujalie, Bwana, kwamba wapewe, katika Jina la Bwana Yesu.

Ndugu wa thamani, Bwana Mungu, naomba usiku wa leo, dhambi zake zikiwa nyingi, jalia zote zisamehewe.

Tujalie, Bwana, ndugu huyu pia.

198 Hivi hutakuja? Njoni kutoka kwenye viti vyenu, ninyi mlio na uvuguvugu sasa, mmerudi nyuma, ama chochote kile. Usilibahatishe, rafiki. Angalieni kile kilichotukia hapa juma hili, mambo ambayo hayajafanywa tangu siku za Yesu wa Nazareti. Inaashiria nini? Wakati wa mwisho umewadia.

199 Kama una baridi kidogo rohoni mwako, kwa nini usije na kusema, "Bwana, ninataka kujiweka wakfu upya. Si—sijafanya mambo niliyopaswa kufanya." Njoni huku pamoja na watu hawa waliosimama hapa.

Hizi hapa familia za watu zinakuja. Hivi hutapanda juu, wewe uliye na uvuguvugu, ama wewe ambaye hujampokea Roho Mtakatifu?

200 Hawa hapa mume na mke vijana wanakuja, wakilia, kijana mwanamume na kijana mwanamke wanakuja; wazee, wakivuta machozi kutoka machoni mwao kwa leso zao. Jambo ndilo hilo.

> Natumaini tu ustahilifu Wako,
> Niutafute uso Wako;
> Iponye roho yangu iliyojeruhiwa, na kuvunjika,
> Loo, niokoe kwa neema Yako.
>
> Mwokozi, Mwokozi,
> Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Usinipite.

201 Hivi hutasimama? Njoni, ninyi mnaomhitaji Kristo. Angalia kile Yeye amefanya juma hili. Kumbukeni, Yeye yupo hapa sasa, hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Mnajua yale niliyofundisha asubuhi ya leo kwenye kiamshakinywa. Roho Mtakatifu, Malaika wa Mungu, yuko papa hapa sasa, na anaendelea kunionya, "Endelea kuita. Mtu fulani yuko huko nje ambaye anapaswa kuja." Njoo. Kumbukeni, sitawajibika kwenye Siku hiyo ya Hukumu.

202 Itengeneze njia yako sasa, kwa sababu Yeye, Bwa—Bwana Mungu, ambaye juma hili ametambua mawazo ya mioyo ya watu, ameninii . . . anaendelea kuniambia, "Endelea kuita, waendelee kuja, kuna mtu huko nje, anayepaswa kuja."

> Mwokozi, . . .

Njoo, ukamtumikie, sivyo?

> Loo, sikiliza kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Loo, usinipite.

203 Sasa, njoni, marafiki. Hatuna "maputo ya peni," na "hatua moja, hatua mbili," tuna hatua moja tu, hiyo ni kusimama kama wanaume na wanawake na kumjia Kristo; njoni mkimwamini Yeye.

> . . . ustahilifu,
> Niutafute uso Wako;
> Iponye roho yangu iliyojeruhiwa, na kuvunjika,
> Niokoe kwa ninii Yako . . .

Njoni sasa, njoni. Waangalie waliosimama hapa.

Mwokozi, . . .

Hii ni ajabu! Njoo wakati maji yametibuliwa.

. . . kilio kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

Inua mkono wako, na useme kutoka moyoni mwako.

Mwokozi, Mwokozi,

Simama sasa. Njoo madhabahuni. Simameni. Njoni huku karibu na madhabahu hapa, na tuombe.

. . . kilio;
Unapozuru wengine,

204 Mtumikie tu Kristo. Tokeni kwenye marefu yenu mshuke. Sema, "Huu hapa utumishi wangu, Bwana, nimekuja kuungama hadharani. Mimi hapa, nimekuwa makosani, Bwana, nimekosea. Nisaidie sasa, nimekuja kuungama dhambi yangu." Njoo! Kila nafsi iliyokandamizwa na dhambi ije.

Mwokozi, Mwokozi,
Loo, sikiliza kilio changu kinyenyekevu;
Wakati . . .

Hiyo ni kweli, Msichana, ulikuwa mmoja wao.

. . . zuru,
Loo, usinipite.

Mwokozi, Mwokozi,

Mtumikie sasa. Njoo huku. Acha machozi ya toba yaje sasa.

Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

205 Vipi kuhusu kila Mkristo hapa ndani? Hebu na tujiweke wakfu kwa Mungu. Kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, simama kwa miguu yako sasa, na hebu tujiweke wakfu kwa Mungu. Njoni karibu, mkiweza. Njoni moja kwa moja huku. Hebu na tujiweke wakfu kwa Mungu, kila mmoja wetu. Sote tunataka kufanya mengi zaidi kwa ajili ya Kristo, kila mtu.

206 Ninajitoa mwenyewe, Bwana, kila kitu nilicho, ninakimwaga katika utumishi Wako. Ninajitoa, Bwana.

207 Kila Mkristo, wajiweke wakfu. Ni kitu gani kilichowafanya ninyi wenye dhambi kuja huku? Mungu aliwaleta hapa juu. Mungu yupo hapa kuziondoa dhambi zenu. Haleluya!

. . . zuru,
Loo, usinipite.

Kila mtu:

Mwokozi, Mwokozi,
Loo, sikia . . .

Huo utavunja michirizi ya barafu, huo utaanzisha uamsho, huo utaiwasha mioto.

Unapozuru wengine,
Usinipite.

208 Sasa, hebu kila mtu na ampe sifa. Tuinue mikono yetu, fungeni macho yenu. Ombeni, ombeni tu mpaka Mungu atakapomimina Roho Mtakatifu juu ya kusanyiko hili, katika Jina la Yesu Kristo. Utukufu kwa Mungu. (Ibada, ichukue sasa.)

62-0630E Mtu Aliye Katili Kuliko Wote Santa Maria
National Guard Armory
Santa Maria, California Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org